SUPA JACKPOT
TZS. 1,117,417,539
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 8

**DART** kuweka mageti umeme kuzuia magari na bodaboda


Nipashe
TESA
Jumanne Mei 23, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI
Ukurasa 12
Mgomo Kariakoo ulivyoibua ari ya kukutana na Waziri Mkuu
Ukurasa 13
Masharti na kukosa mbinu utafutaji kunavyowakwamisha wenye ulemavu
Ukurasa 14
Zinaibuliwa mbinu kurejesha wasiopenda shule darasani
ELIMU
NA MARCO MADUHU, SHINYANGA
Mwanandoa hili ni somo mikopo umiza, komaa usifilisiwe, simama na sheria
Wanafamilia wanaweza kulala nje baada ya nyumba kutwaliwa na watoa mikopo umiza. PICHA: MTANDAO

Jumanne Mei 23, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581319
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11



MAZUNGUMZO MAALUM

## Dk. Slaa: Kina Mdee watoke bungeni

**ATOA** angalizo ufisadi, katiba mpya... *Endelea ukurasa 3*


# Ni mwaka wa miundombinu

UKURASA 2



- BARABARA ZA KUUNGANISHA MIKOA, WILAYA KUJENGWA KM 2,035
- VIWANJA VYA NDEGE VYATENGEWA MABILIONI
- BARABARA ZA JUU (FLYOVERS) SASA KILA KONA DAR ES SALAAM
- WANAWAKE KUPEWA KIPAUMBELE ZABUNI ZA MIRADI
- TRILIONI 1.113/- ZAELEKEZWA SGR. WANANCHI KULIPWA FIDIA
- MALIPO NDEGE MPYA 3, KUTOA 'ADVANCE' NDEGE MPYA 2
- MELI, VIVUKO VICHEKO, TMA KUNUNULIWA RADA MPYA NNE

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24 bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


TANZANIA-CHINA FRIENDSHIP TEXTILE CO. LTD
UBUNGO, DAR ES SALAAM
Kumb. Na.: 2/116/VOL. VI-B/86
Tarehe: 5.5.2023
Kwenda kwa:
WAFANYAKAZI WOTE,
TANZANIA-CHINA FRIENDSHIP TEXTILE CO. LTD.,
S.L.P. 20842,
DAR ES SALAAM.

KWA: WAFANYAKAZI WOTE

YAH: NOTISI KUHUSU MAHITAJI YA UENDESHAJI
*Chini ya Kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, 2004 na Kanuni 23(4) ya Utendaji Bora Kazini T.S. Na. 42/2007*

Pata taarifa kwamba kwa mujibu wa Kifungu cha *38(1) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, 2004 na Kanuni 23(4) ya Utendaji Bora Kazini T.S. Na. 42/2007*, mwajiri anawajibika kutoa notisi mapema zaidi kwa wafanyakazi endapo anakusudia ... Kupunguza Wafanyakazi kwa mahitaji ...

RIPOTI YA UCHUNGUZI

## Wafanyakazi 200 Urafiki kufutwa kazi, kiwanda sasa kufungwa

UKURASA 4

**MICHEZO** RAIS SAMIA ANUNUA TIKETI 5,000 YANGA UK. 24 **KATUNI** UK. 6



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) kilichofanyika ukumbi wa Halmashauri Kuu (White House) Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Ni mwaka wa miundombinu

**Na Romana Mallya,**
DODOMA

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi imetangaza kuwa katika mwaka ujao wa fedha, itajenga barabara zenye urefu wa Km 2,035 kwa kiwango cha lami na kuendelea na utekelezaji wa miradi mikubwa ya reli ya kisasa, ununuzi wa ndege na madaraja, likiwamo daraja la juu la Jangwani jijini Dar es Salaam.

Pia imepanga kununua rada nne kwa ajili ya Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), kujenga vivuko na kuimarisha sekta ya anga kimiundombinu.

Akiwasilisha jana bungeni jijini hapa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka huo wa fedha, Waziri wake, Prof. Makame Mbarawa, aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 3.554 kwa ajili ya utekelezaji wa mikakati hiyo.

Kati ya fedha hizo, Sh. trilioni 1.468 ni kwa ajili ya sekta ya ujenzi na Sh. trilioni 2.086 za sekta ya uchukuzi.

Prof. Mbarawa alisema ndege mbili aina ya Boeing 737-9 zinatarajiwa kuwasili mwishoni mwa Agosti na Desemba mwaka huu na moja ambayo ni Boeing 787-8 Dreamliner inatarajiwa kuwasili Februari, mwakani na watasimika mfumo wa kuhudumia abiria katika viwanja vya ndege vya Mwanza, Bukoba, Arusha, Songwe na Dodoma.

Alisema wataendelea kutekeleza mradi wa kununua na kufunga rada nne za hali ya hewa na mbili tayari zikiwa zimepokewa na kazi ya ufungaji inaendelea katika mikoa ya Mbeya na Kigoma.

Waziri huyo pia alisema watalipa madeni ya makandarasi na wahandisi washauri, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani, upanuzi na ujenzi wa barabara na madaraja pamoja na ujenzi wa vituo vya ufuatiliaji na uokoaji.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24, barabara saba zenye jumla ya urefu wa Km 2,035 zitajengwa kwa kiwango cha lami kwa kutumia utaratibu wa EPC + F.

Alizitaja barabara ni za Kidatu-Ifakara-Lupiro-Malinyi- Kilosa kwa Mpepo-Londo-Lumecha/Songea (Km 435); Karatu-Mbulu-Haydom-Sibiti River-Lalago-Maswa (Simiyu) (Km 339); Handeni-Kibirashi-Kijungu-Kibaya-Njoro-Olboroti-Mrijochini-Dalai-Chambalo-Chemba-Kwa Mtoro-Singida (Km 460).

Nyingine ni Arusha-Kibaya-Kongwa Junction (Km 453.42); Masasi-Nachingwea-Liwale (Km 175); Igawa-Songwe-Tunduma (Km 218) pamoja na barabara ya mchepuo ya Uyole-Songwe Km 48.9; na barabara ya Mafinga-Mtwango-Mgololo (Km 81).

Vilevile, alisema wizara itaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Kibaha-Chalinze-Morogoro (Km 205) ya kiwango cha Express Way kwa kutumia utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi (PPP).

Waziri Mbarawa alisema miradi mingine ya barabara kwa kiwango cha lami na madaraja itakayotekelezwa ni barabara ya Soni-Bumbuli-Dindira-Korogwe (Km 74), Mtwara-Newala-Masasi (Km 210), Likuyufusi-Mkenda (Km 122.5), Ubena Zomozi-Ngerengere (Km 11.6).

Vikawe-Mapinga (Km 24), Makofia-Mlandizi (Km 36.7), Makofia-Mlandizi, Musoma-Makojo-Busekela (Km 92) na Kongwa-Mpwapwa-Gulwe-Kibakwe (Km 98), Muhutwe-Kamachumu-Muleba (Km 54), Iringa-Ruaha National Park (Km 104) na Iringa (Ipogolo)-Kilolo (Km 33.2).

Pia zimo barabara za Muheza-Amani (Km 36), Mtwara-Mingoyo-Masasi (Km 200.51), Kibaoni-Majimoto-Muze-Kilyamatundu (Km 189).

**MADARAJA**

Prof. Mbarawa alisema Sh. bilioni 15.162 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi (J.P. Magufuli), barabara unganishi na maandalizi ya ujenzi kwa Daraja la Mzinga Sh. milioni 250 na Daraja la Ugalla Sh. milioni 500.

Alisema Daraja la Kitengule na Barabara Unganishi limetengewa Sh. milioni 3,010 kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya mkandarasi na mhandisi mshauri wa ujenzi.

Prof. Mbarawa pia alisema Sh. milioni 61,585 zimetengwa kwa ajili ya barabara za mikoa na madaraja katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

Alisema mradi wa kupunguza msongamano Dar es Salaam umetengewa Sh. milioni 10,190 kwa ajili ya kulipa madeni ya makandarasi wa barabara mbalimbali mkoani humo.

**BARABARA ZA JUU**

Waziri huyo alisema mradi ujenzi wa barabara za juu (Flyovers) mkoani Dar es Salaam na barabara unganishi umetengewa Sh. milioni 320 fedha za ndani na Sh. milioni 1,100 fedha za nje kwa ajili ya kulipa madeni ya makandarasi na wahandisi washauri katika makutano ya Ubungo (Ubungo Interchange) pamoja na kuendelea na maandalizi ya kuboresha makutano ya barabara ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco, Buguruni, Mbezi Mwisho, Fire na makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Jct).

Kuhusu miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT Phase I - V: Km 69.8), Prof. Mbarawa alisema Sh. milioni 2,255 fedha za ndani na Sh. milioni 42,630 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu Awamu ya Pili.

Vilevile, wataendelea na ujenzi Awamu ya Tatu na Nne, maboresho ya miundombinu Awamu ya Kwanza na kuanza ujenzi wa Daraja la Jangwani na miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tano.

**VIWANJA NDEGE, SGR**

Waziri huyo alisema miradi ya miundombinu ya viwanja vya ndege imetengewa Sh. milioni 96,830 ikihusisha ujenzi, ukarabati, uendelezaji na umaliziaji wa viwanja vya ndege vilivyopo mikoa mbalimbali.

Alisema miradi ya ruzuku itatekelezwa na Wakala wa Fundi na Umeme Tanzania inayohusisha maegesho ya vivuko, ukarabati na ujenzi wa vivuko vipya na ujenzi na ukarabati wa karakana.

Alisema Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetenga Sh. bilioni 40.1 ili kudhibiti huduma za usafiri ardhini na Sh. trilioni 1.113 zinatarajiwa kutumika kugharamia ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), ununuzi wa injini na mabehewa ya mizigo na abiria na upembuzi yakinifu kwa ajili ya miradi ya reli.

"Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) limetengewa Sh. bilioni 1.73 fedha za nje kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Sh. bilioni 70.905 miongoni mwa kazi itakazofanya ni ujenzi wa Kituo cha kikanda cha kuratibu Utafutaji na Uokozi Ilemela, Mwanza (MRCC); ujenzi wa vituo vitatu vya Kitaifa vya Utafutaji na Uokozi na ununuzi wa boti mbili za utafutaji na uokozi pamoja na boti moja ya matibabu," alisema.

Pia alisema Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) imetenga Sh. bilioni 820.03 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo upanuzi wa kina na upana wa lango kuingilia na kugeuzia meli.

**SEKTA YA ANGA**

Alisema serikali imepanga kutumia Sh. bilioni 271 kukamilisha malipo ya kimkataba ya ununuzi wa ndege tatu mpya (ndege moja aina ya Boeing 787-8 Dreamliner na mbili aina ya Boeing 737-9. Pia kufanya malipo ya awali kwa ajili ya ununuzi wa ndege mpya aina ya Boeing 737-7 na DeHavilland Q400 moja.


**UBALOZI WA CANADA, UINGEREZA, DENMARK NA WATAALAM MBALIMBALI DAR ES SALAAM**

**MNADA WA HADHARA**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Canada, Uingereza, Denmark na Wataalam mbalimbali watauza kwa mnada wa hadhara Fanicha na Magari tarehe 27 Mei, 2023 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

Fanicha zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi: Sofa set, Sofa bed, China base/Hutch, Chest drawer, Dresser, Book case, Buffet, Dining Table, Chairs, Office Desk, Big File cabinet set mounted on rails, Vitanda, Magodoro, Fridge double door, Deep Freezer, Washer, Garden table / chair, Computer set, TV Set, Music systems, Photo copy m/c, A/C split units, Trade Mill, Big Satellite dish complete, Scafolding unit, Automatic Incubator, Water pumps etc.

**Vehicles Bidding Start at 12:00 hrs**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ford Ecosport Station Wagon | FY58 - Petrol Engine | 2015 | Haujalipwa |
| 1 | VW Amarok TDI Pickup Double Cabin | CNE Diesel Engine | 2012 | Umelipwa |
| 1 | Nissan Murano Station Wagon | VQ35 Petrol Engine | 2006 | Umelipwa |
| 1 | ISUZU Mobile Cold room 4 Tons | 6HH Diesel Engine | 1997 | Umelipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia t**arehe 24 mpaka 26 Mei 2023, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.**

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 5 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 2 June, 2023 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB na NBC yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini.

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE DAR ES SALAAM**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926**

**E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

HABARI KITAIFA

# Slaa: Kina Mdee watoke bungeni

**Enock Charles na Zanura Mollel**

ALIYEKUWA Balozi wa Tanzania Sweden, Wilbroad Slaa, amesema haoni sababu inayowezesha wabunge 19 wanaoongozwa na Halima Mdee kuendelea kuwapo bungeni ilhali chama chao kilishafanya uamuzi dhidi yao.

Dk. Slaa aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), alitoa kauli hiyo jana wakai wa mazungumzo maalum na Nipashe nyumbani kwake mkoani Dar es Salaam.

Alisema wabunge hao hawatakiwi kuwapo bungeni kwa kuwa hawana ridhaa ya CHADEMA na hakuna zuio la kisheria la kuwafanya kuendelea kuitwa wabunge wa viti maalum.

Mdee na wenzake walifungua shauri namba 36/2022 Mahakama Kuu Julai 22, 2022, wakiomba mahakama ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Katika shauri hilo, wabunge hao wanaiomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama, iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza na kuwekwa zuio kwa Spika wa Bunge na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuchukua hatua yoyote hadi malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.

Katika mazungumzo na Nipashe, Dk. Slaa alisema anatambua uwezo wa baadhi ya wabunge hao, akiwatolea mfano Mdee, Ester Bulaya na Ester Matiko kwamba lishiriki kuwajenga. Ni kazi kubwa kujenga wengine wa mfano wa hao. Itachukua muda mrefu, lakini utaratibu uliotumika kuwaweka bungeni ni wa kibabe.

"Kwa muda mrefu nimekuwa ninakwepa kujibu hili swali kuhusu kina Halima Mdee. Sababu ya kutojibu ni kwamba mimi kichwani kwangu ninashindwa kuamini kwamba wale wanawake wameenda bila mtu fulani kupeleka majina. Kwa hiyo, nilikuwa ninatafuta. Pili, kwamba huenda walizungukana huko ndani (CHADEMA).

"Nikawa pia ninashindwa kumbana Spika kwa sababu kwa kawaida yeye anapelekewa majina na NEC. Kwa hiyo, nikategemea katika kipindi chote wanabishana atajitokeza mtu aseme kuna aliyeghushi, lakini hakuna aliyetokeza. Nikategemea atajitokeza wa kusema tume haikupeleka majina lakini hakuna aliyetokea.

"Nikategemea kuna atakayehoji Spika ndiye aliyekosea, lakini Spika ameendelea kulalamikiwa kuwa alipelekewa barua haraka baada ya uamuzi wa Baraza Kuu.

"Na wakati huo anapelekewa barua hapakuwa na zuio, nikafuatilia kesi mahakamani, hakuna yeyote anayehusika na haya niliyoyataja. Kesi iliyopo ni kuomba mahakama kwamba CHADEMA iwape fursa ya kuwasikiliza, hayo niliyoyataja yote hakuna hata moja lililopo mahakamani.

"Baada ya kuzingatia hilo, hoja inayokuja ni kwamba kama haya makubwa niliyoyataja hayakuhojiwa, tafsiri pekee iliyopo ni kwamba wakati CHADEMA ilipothibitisha uamuzi wa Kamati Kuu wa kuwafukuza hapo katikati wakati huo hakuna chochote mahakamani na hapakuwa na pingamizi la Spika kuwaondoa. Kwa hiyo, ni kiburi tu cha Spika, hakutaka kuwaondoa.

"Spika ametafuta tu kisingizio watu wasioelewa wanaamini kwa kuwa kuna kesi iliyopo mahakamani, lakini wanashindwa kuunganisha ile kesi ni ya nini, ile kesi unataka tu wao kurudishiwa nafasi ya kwenda kusikilizwa. Sasa hiyo inahusiana nini na wao kuwapo bungeni?" alihoji Dk. Slaa.

**KATIBA MPYA**

Kuhusu hoja ya katiba mpya, Dk. Slaa alisema anaona hakuna nia ya dhati ya kupatikana katiba ya wananchi kwa kuwa hadi sasa hakuna hatua muhimu zilizochukuliwa ikiwamo kutengwa bajeti ya kuanzishwa mchakato huo.

"Tumeona kilichotokea mwaka 2019 na 2020, viongozi karibia wote hawajachaguliwa na wananchi. Sasa kwa sisi tunaojua nini maana ya uchaguzi, hiki kitu hatuwezi kukikubali.

"Ninajua kuna watu walisema kwani katiba inaleta chakula mezani? Huo ni upuuzi, ni fikra potofu, hakuna kitu duniani ambacho hakifanywi na katiba, nenda Marekani, Rais mstaafu ambaye sisi tunamlinda kwenye Katiba kule anashtakiwa.

"Nchi kama Marekani Rais hawezi kujiamulia tu kwa kuwa yeye ni Rais, hata Deni la Taifa kulipwa ni mpaka idhini ya Bunge. Juzi hapa Joe Biden akiwa katika Mkutano wa G7 wabunge wamemwambia imefika muda wa kulipa Deni la Taifa na tusipolipa tutaingia kwenye matatizo, amerudi haraka. Je, hapa Tanzania Kamati ya Bunge inaweza kumwita Rais kumwambia chochote?" Alihoji.

Dk. Slaa pia alizungumzia ubadhirifu wa mali ya umma uliotajwa katika ripoti mpya ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

# Ajali zilivyoua sita, kujeruhi 13 Tabora

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WATU sita wamefariki dunia na wengine 13 kujeruhiwa katika ajali ya gari na bodaboda mkoani Tabora.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Costantine Bugambi, amethibitisha kuwapo kwa ajali hizo. Zilitokea Mei 21 na 22 saa 12:45 asubuhi zikihusisha pikipiki, basi na Toyota Land Cruiser, mali ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita.

Alisema ajali ya kwanza ilitokea Kijiji na Kata ya Ililangulu wilayani Uyui. Basi la Kampuni ya Dilaix aina ya Tata namba T 164 DEL liligongana na lori aina ya Scania namba T584 DTL na kusababisha vifo vya watu wanne akiwamo na dereva wa lori hilo huku wengine 13 wakijeruhiwa.

Ajali nyingine ilitokea Mei 22 saa tisa alasiri. Toyota Land Cruiser mali ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Geita yenye namba za usajili wa STL 9690, kumgonga dereva wa pikipiki namba MC 483 BVL na kusababisha kifo chake.

Alisema kuwa watu 13 waliojeruhiwa walikimbizwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tabora kwa ajili ya matibabu huku wengine wakiruhusiwa baada ya kupata nafuu.

Alisema mwili wa dereva wa pikipiki umehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Nzega na madereva wawili wanashikiliwa na polisi mkoani humo kwa uchunguzi zaidi.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## OMBI LA KUONESHA NIA YA UTOAJI WA HUDUMA YA USIMAMIZI WA WAKUFUNZI WAKATI WA PROGRAMU YA MAFUNZO KUMBUKUMBU NA. 00000240

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Ltd, ("EACOP LTD") inakaribisha kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha ili kuonesha nia ya kutoa Huduma za Usimamizi wa Mafunzo kwa Wakurufunzi katika kipindi cha programu ya mafunzo.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta ghafi lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi kwenda katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani, karibu na mji wa Tanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

Kwa niaba ya EACOP Ltd, mkandarasi atakayechaguliwa, atasimamia wakurufunzi ambao watapatiwa mafunzo ya kiufundi kwa awamu mbalimbali kwenye vituo vya mafunzo vilivyochaguliwa. Programu ya mafunzo itaendeshwa kwa kipindi cha kati ya miezi 24 hadi 30. Mkandarasi aliyechaguliwa atatekeleza shughuli za usimamizi kwa wakurufunzi zikiwemo shughuli mahususi zifuatazo:

- Kufanya tathmini na mapatio ya utimamu au uimarifu wa afya pale inapohitajika na EACOP ltd hii haitajikita kwenye upimaji wa utimamu au uimarifu wa afya tu, bali pia kuratibu utoaji huduma za upimaji wa UVIKO 19 pamoja na huduma za vipimo vingine vya kiafya.
- Kuhakikisha kuwa wakati wote wa mkataba, Wakurufunzi wanaopatiwa mafunzo wanakuwa na maadili mema na afya njema pamoja na uwezo mzuri wa kumudu kutekeleza majukumu yao.
- Kutoa huduma za usimamizi na uratibu, ambazo zinajumuisha usafirishaji, huduma za matibabu kwa wakurufunzi pamoja na maadili mema na afya ya kimwili, pamoja na uidhinishaji wowote wa kiutawala unaojumuisha vibali vya kazi, na/au viza za kikazi zinazohitajika.
- Kulipa mshahara wa kila mwezi, posho, tozo zinazotakiwa pamoja na bima, kwa ujumla kulipa gharama zote za moja kwa moja au zisizo za moja kwa moja zinazowahusu wafanyakazi waliotajwa, pamoja na gharama mbalimbali za Kodi na ushuru husika.
- Kuandaa mahitaji ya safari kwa ajili ya wakurufunzi pale inapohitajika.
- Kutoa wafanyakazi wenye sifa stahiki kwa nafasi mbili za Mshauri wa Wanafunzi na Msaidizi wa Masuala ya Kiutawala. Wote watafanya kazi mahali ambapo mafunzo yatakuwa yanafanyika.
- Kutoa vifaa vya Teknolojia ya Mawasiliano kwa WAKURUFUNZI kwa kuzingatia viwango na mahitaji ya EACOP ltd.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Makampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo**

- Leseni ya biashara.
- Leseni halali, kama ipo, kutoka mamlaka ya ndani ya nchi husika kwa ajili ya utoaji wa huduma husika.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi kwa mwaka wa fedha uliopo.
- Cheti cha usajili au maombi yaliohidhinishwa ya usajili kwenye kanzi data ya Watoa Huduma ya Ugavi wa Ndani (LSSP) ya EWURA wakati wa kuonesha nia.
- Kukidhi vigezo vya Kanuni ya Maudhui ya Wazawa za mwaka 2017
- Wasifu wa wafanyakazi muhimu watakaohusika katika mradi ikiwa ni pamoja na vyeti vya lazima vya wahudumu na viwango vya elimu, pamoja na uzoefu na uwezo wa kutoa huduma zinazotakiwa
- Nyaraka zinazoonesha uzoefu, utendaji na uwezo wa kutoa Huduma kwa maeneo yaliyoorodheshwa hapo juu katika kiwango kikubwa nchini Tanzania, kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi kama hii.
- Uthibitisho wa sera za kupinga rushwa, ufisadi, na kuzingatia Haki za Binandamu

Makampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com**, (ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb**). Maombi yatumwe ifikapo au kabla ya saa **11:00 jioni** kwa saa za Africa Mashariki (EAT) ya mnamo tarehe **21 Juni 2023**. Kichwa cha Barua pepe kiwe: **00000240 - Utoaji wa Huduma za Wakurufunzi wa Utawala.**

Maombi yote ya kuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20

Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini makampuni yatakayojumuishwa kwenye orodha ya (Makampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Kampuni zilizofuzu hatua ya awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika

## KUYUMBA UCHUMI VIWANDA -2

# Wafanyakazi 200 kuondolewa Urafiki ili kufunga kiwanda

**Na Mwandishi Wetu**

***KATIKA** sehemu ya kwanza jana, tuliona hujuma zilizofanyika Urafiki, kasi ya kubadilisha matumizi ya eneo husika kutoka kiwanda hadi ghala, maegesho, kumbi za starehe, ofisi na nyumba za ibada. Endelea...*



Mwonekano wa nyumba za wafanyakazi wa Kiwanda cha Nguo cha Urafiki kilichopo Dar es Salaam ambazo zinageuzwa ofisi, maegesho ya magari huku eneo la kiwanda likiwa ni maghala ya kuhifadhia bidhaa za wafanyabiashara na wachuuzi kutoka China. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Nipashe ilizungumza na wafanyakazi wastaafu na waliopo kazini ambao wanashangaa kinachoendelea na kujiuliza juu ya nia ya serikali kuwa na viwanda kwa kutumia malighafi za ndani kama pamba na kuacha kuwa soko la nguo kutoka nje hasa China ambaye ndiye mwekezaji mwenza.

Aidha, wanasema wanashangazwa na mabadiliko yanayofanywa na serikali bila kuwashirikisha hatua ambazo wanaona hazitafsiri nia ya kuwa na kiwanda cha nguo ambacho kilikuwa cha pekee Afrika Mashariki.

Aliyekuwa msimamizi wa idara ya uandisi mitambo, Seif Mbuva, anasema aliajiriwa mwaka 1980 akiwa na miaka 20 amefanyakazi kwa miaka 30, aliona hatua zote hadi kiwanda kinakufa huku akiambulia fedha kinua mgongo kisichozidi Sh. milioni moja na mafao ya Sh. milioni 3 huku pensheni ya mwezi ni Sh. 100,000.

Anasema eneo alilokuwapo kazi yao ilikuwa ni kuchemsha maji na kupata mvuke kwa ajili ya eneo la uchapaji, kukausha nguo na kulainisha zikishatoka kwenye mitambo.

"Nilivyoanza kazi kulikuwa na mzunguko mara nne yaani asubuhi siku mbili, mchana siku 2 na usiku siku mbili halafu wanapumzika siku mbili, ambazo zilipungua hadi ikabaki moja kutokana na uzalishaji kupungua,"anasema na kuongeza:

"Uzalishaji uliyumba, niliona Wachina wakileta vitambaa kwa ajili ya kichapisha, Sijaelewa mkataba kati ya serikali na China ulikuwaje, uendeshaji wa kiwanda na mambo yalivyokuwa yanakwenda nasi tulikuwa tunashangaa, tuliona hujuma na hakuna hatua zilizochukuliwa,"anasema.

"Tusichoelewa tunaona kuna Mchina mmoja anasimamia kwa kuwa wao walikuwa na hisa 51, sijui kwanini kiwanda hakiendelei," anasema Mbuva aliyekuwa anashona nguo nje ya kibaraza eneo la Urafiki.

Mbuva anasema nchi yote haiwezi kuendelea bila viwanda hasa vya nguo, hivyo anaiomba serikali kuhakikisha vinafanyakazi, ili kutoa ajira kwa wingi kama ilivyokuwa miaka ya zamani kuliko kugeuza eneo hilo kuwa ofisi, gereji na maegesho ya magari.

Mfanyakazi Neema John anasema kiwanda kilisaidia ajira kwa kuwa watu zaidi ya 3,000 walipata ajira, lakini kwa sasa kimekufa vijana wanahangaika kiasi cha wengine kuwa vibaka na kuongeza idadi ya wasiokuwa na kazi nchini.

"Nilianza kazi mwaka 1991 kabla ya ubinafsishaji eneo la usokotaji wa nyuzi, niliendelea kujisomea kwenye Chuo cha Textlile Technology kilikuwa ndani ya kiwanda, nilivyohitimu nikahamishiwa eneo la teknolojia kazi yangu kupima ubora wa pamba,"anasema.

"Kwa sasa hakuna kitu, tunakwenda kufanya usafi tunakaa, tunasubiri kustaafishwa. Serikali ifufue hiki kiwanda, enzi hizo nguo ya Urafiki ni pamba asilimia 100, kwa sasa kanga ni 'polista' na ndogo hazifai kabisa," anasema.

Evarest Mzava anasema aliajiriwa mwaka 1988 kwa mshahara wa Sh. 35,000 (sasa analipwa 190,000) kiwanda kikiwa katika hali nzuri hadi mwaka 1994 kiliyumba, na wafanyakazi walikwenda likizo ya miaka miwili bila malipo, ili kupunguza matumizi, na wachache waliobaki walikuwa wanakopa malighafi ili kiwanda kisife.

"Serikali ilitafuta mbia, 1997 wafanyakazi wote waliokuwa likizo walilipwa stahiki zao, mimi nililipwa Sh. 400,000 ikiwa ni makadirio ya kustaafishwa kwa mshahara wa Sh. 17,000," anabainisha.

**HUJUMA**

Anasema baada ya mwekezaji kuja aliona hujuma ikiwamo kuuza mitambo kama vyuma chakavu, matumizi ya maji ya visima yaliyoua mitambo, kung'olewa mashine kwa ahadi ya kuleta mpya ambazo hadi sasa hazijaletwa.

Yote haya tulijulisha serikali lakini hakuna hatua zilizochukuliwa, sisi ndio tulikuwa wafanyakazi tunanufaika na ajira lakini wenzetu (serikalini) wala hawakuona uchungu na kuchukua hatua hadi sasa eneo limebaki kama gofu.

"Unajua siyo rahisi mtu mwenye viwanda vya nguo anayetengeneza ili akuuzie wewe aendeleze kiwanda chako nyumbani kwako (nchi) wakati anataka uwe soko la bidhaa zake atengeneze ajira nchini kwake.

"Baada ya kuuza mitambo akaanza kuleta nguo zilizotengenezwa China ambazo hazina ubora hata ukubwa wake hautoshi, ndiyo mwanzo wa soko la Urafiki kuharibika," anasema Mzava.

Anasema baada ya muda mwekezaji alitaka atulipe Sh. 80,000 nasi tulitaka mshahara wa kima cha chini na kwamba waliishi kwenye migogoro hadi siku moja waliwafungia nje uongozi.

**LAWAMA SERIKALINI**

Anasema: "Kwa maoni yangu serikali inaua vitu vyake yenyewe, sisi tumelalamika tumewapelekea taarifa na ushahidi wote na kutoa taarifa ya hujuma, lakini haichukui hatua hii ni sawa na kuua viwanda vyake yenyewe nasi tunakosa ajira."

Anasema: "Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alikuja kiwandani akatuambia msieleze lolote kila kitu nakijua nitakwenda kufanyia kazi, tangu ameahidi atarudi hajarudi hadi leo ni miaka mitano."

Kauli ya mfanyakazi huyo inaungwa mkono na Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi Tawi la TUICO, Saidi Mteje, anayesema mwaka 2018 Waziri Mkuu, Majaliwa alitembelea kiwanda hicho na kutoa maelekezo mengi na wafanyakazi waliandika hoja zao, lakini aliwaambia matatizo yote anayajua hawana haja ya kumkabidhi maandishi.

"Alituambia poleni sana, Rais Dk. John Magufuli (rais wakati huo) anajua matatizo ya hapa na anawapa pole, akatuomba tusiwe na wasiwasi kwa kuwa kila kitu kiko serikalini. Tulijitahidi tuliyoyaandika tukayapenyeza kwa wasaidizi wake ili waone wanakokwenda kama watayafanyia kazi,"anasema na kuongeza:

**PM AENDA KUFUTURU**

"Waziri Mkuu aliongea sana baadaye akasema "Nakwenda kufuturu namuachia maagizo Waziri wa Viwanda na Uwekezaji (wakati huo), Charles Mwijage, atekeleze yote na majibu niyapate saa 12 ili tujue serikali inachukua hatua gani."

Tangu ameondoka mwaka huo ameenda kufuturu na hajarudi hadi leo, hadi sasa hatujapata taarifa yoyote ya serikali, wamebadilishwa mawaziri mara tatu wa viwanda lakini hakuna anayezungumzia Urafiki," anafafanua.

"Hatujui kama kiwanda kitafufuka au la, ubia uliopo utaendelea vipi, tunaona umebaki kinadharia," anasema Mteje.

**WAFANYAKAZI WALIOBAKI**

"Mashine zilizoingia maji ya chumvi kwa sasa zimekuwa udongo ukishika vinapukutika. Ili kifufuke kiitwe Urafiki inabidi mitambo iliyopo ndani iondolewe, mapaa yanavuja kama chekechea vinginevyo ni historia," anasema.

Aidha, anasema raia wa China wanaoingia kwenye eneo la kiwanda ambako kuna maghala dawa na pamba yamepangishwa kwenye maghala.

**MASWALI MAGUMU**

Nipashe imebaini kuwa hivi karibuni serikali ilitoa notisi ya kuwaondoa wafanyakazi 200 kiwandani hapo, kwa kile kilichoelezwa kuwa ni uamuzi wa bodi ambayo wafanyakazi wanadai hawaifahamu na haipo.

Wanasema kampuni ina madeni makubwa lakini nani amesababisha madeni hayo? Aliyesababisha alichukuliwa hatua gani? Madeni hayo yanawahusuje wafanyakazi? Kwanini hakuna mapato na matumizi?

"Unapowaondoa wafanyakazi ni lazima uwape taarifa baada ya kukaa kikao na wafanyakazi lakini hapa tunaona wameleta barua ya kusudio la kuondoa wafanyakazi 200 maana yake ni wote kwa sababu tuliobakia ni 158," alidokeza mmoja wa wafanyakazi.

Mwandishi anafahamu kuwapo notisi iliyotolewa na Kaimu Naibu Meneja Mkuu wa kiwanda hicho, Thomas Mushi, ya Mei 5 mwaka huu, ikieleza kusudio la kupunguza wafanyakazi na kuwataka wafike katika kikao Mei 9, mwaka huu. Kikao hicho kilivunjika. Kikao kingine kimepangwa kufanyika leo kiwandani huko.

Alipoulizwa kuhusu madai hayo, Mwenyekiti wa TUICO tawi la kiwandani, Saidi alisema ni kweli walipokea barua ikieleza kusudio la kuwapunguza kazi, na kwamba wanataka haki itendeke kwa kuwa madai mengi ya wafanyakazi waliostaafu hayajakamilika ikiwamo michango kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

"Mtu amefanyakazi miaka 30 anakwenda kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii anaambiwa michango iliyopelekwa ni Sh. 50,000 au 100,000, hii siyo haki kabisa,"alisema.

**MENEJA, MSAJILI HAZINA**

Nipashe ilimtafuta meneja wa kiwanda hicho, Mushi ambaye alisema hawezi kuzungumza kwa kuwa kiwanda kiko chini ya Msajili wa Hazini ambaye ndiye msemaji wa kila kitu.

Kuhusu mabadiliko yanayoendelea alisema "Ni kweli tumepangisha kama unavyoona ili tupate kodi ya kuendesha eneo hili, hatuwezi kuliacha likae lilivyo wakati tunaweza kupata mapato.

Ofisi ya Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu, ilipelekewa maswali Machi 22, mwaka huu, kupitia ofisa habari ambayo hayajajibiwa.

***Itaendelea......***

## RC awataka waajiri kujisajili, kuwasilisha michango WCF

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, amewataka waajiri kujisajili na kuwasilisha michango katika Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kwa manufaa ya wafanyakazi pindi wakipata changamoto za kuumia au kuugua kutokana na kazi.

Alitoa rai hiyo jana jijini hapa kupitia hotuba yake iliyosomwa na Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masalla, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku tano ya tathmini za ulemavu uliosababishwa na ajali na magonjwa yatokanayo na kazi kwa madaktari wa mikoa ya Kanda ya Ziwa, ikijumuisha Mwanza, Kagera, Mara, Simiyu, Geita na Shinyanga.

"Ili unufaike na huduma au mafao yanayotolewa na WCF, ni lazima waajiri wajisajili na kuwasilisha michango ya wafanyakazi waliowaajiri," alifafanua.

Alisema kuwa kwa sasa wafanyakazi wanao uhakika wa kinga na kipato kutokana na majanga yanayosababishwa na ajali, magonjwa na vifo kutokana na kazi kufutia kuwapo WCF.

"Waajiri nao wanapata muda zaidi wa kushughulikia uzalishaji na uendelevu wa biashara zao na hivyo kuongeza tija inayopelekea kuongezeka kwa pato la taifa," alisema.

Aliwataka washiriki kuwa waadilifu wanapotekeleza jukumu hilo la kufanya tathmini ya ulemavu utokanao na ajali au magonjwa yatokanayo na kazi ili WCF itoe fidia stahiki na kwa wakati.

Alisema kuwapo mfuko huo ni hatua mwafaka katika mazingira ya sasa ambapo serikali inaendelea na kazi ikiwamo kujenga uchumi na hivyo kuwa na ongezeko kubwa la maeneo ya uzalishaji.

"Katika hali ya kawaida ongezeko la kazi litakwenda sambamba na ongezeko la matukio na athari zinazotokana na ajali na magonjwa yatokanayo na kazi, hivyo jukumu la WCF sio kulipa fidia pekee bali pia kushirikiana na wadau katika kubuni na kuendeleza mbinu za kupunguza au kuzuia ajali na magonjwa yatokanayo na kazi," alisisitiza.

Awali akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Mkurugenzi wa Huduma za Tathmini WCF, Dk. Abdulsalaam Omar, alisema mafunzo hayo ni sehemu ya hatua muhimu ya kuuwezesha mfuko kutekeleza vyema jukumu la kufanya tathmini sahihi na hatimaye kutoa fidia stahiki pindi mfanyakazi anapoumia au kuugua kutokana na kazi.

"Kwa mwaka huu wa fedha tayari tumetoa mafunzo kwa madaktari 85 na leo (jana) tunawafundisha madaktari 100 na hivyo watafanya idadi ya madaktari ambao tayari wamepatiwa mafunzo na WCF ya kufanya tathmini za ulemavu uliotokana na ajali na magonjwa yatokanayo na kazi kufikia 1,585 nchi nzima," alifafanua Dk. Omar.

RIPOTI YA LHRC

# Mabadiliko tabianchi yameingilia haki ya faragha baadhi ya familia

**Na Sabato Kasika**

RIPOTI mpya ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi, imebaini baadhi ya familia kuikosa haki ya faragha.

Ibara ya 16(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inatamka "kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake na unyumba wake, pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake ya binafsi."

Ripoti hiyo ya LHRC iliyopewa jina la 'Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Kwenye Haki za Binadamu', imebainisha kuwa mbali na kusababisha shida katika haki ya faragha, pia kuna athari za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni katika baadhi ya mikoa nchini.

Katika uzinduzi wa ripoti hiyo mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, alisema kituo kimefanya utafiti katika kanda nne za Tanzania Bara ambazo ni Kati, Pwani, Kaskazini na Ziwa na kubaini athari hizo.

"Kanda hizo zinajumuisha mikoa ya Pwani, Dodoma, Manyara, Mwanza, Dar es Salaam, Kagera na Mbeya. Utafiti uliangazia kilimo, ufugaji, uvuvi na makazi ya watu," alisema Dk. Anna.

Mkurugenzi huyo alifafanua kuwa utafiti huo ulifanyika kwa miezi mitano kuanzia Julai hadi Novemba mwaka jana, ukihusisha wilaya 10 na vijiji 20 katika mikoa hiyo sita na kuibuka na matokeo hayo.

"Ripoti hii ya mabadiliko ya tabianchi na athari zake kwenye haki za binadamu, imebaini baadhi ya mambo yanayoonekana dhahiri kuathiriwa na mabadiliko hayo," alisema Dk. Anna.

Aliyataja baadhi ya mambo hayo kuwa ni afya, upatikanaji wa majisafi, mazingira kwa ujumla wake na kukosekana kwa usawa kwa kuwa wanaoteseka zaidi wakati wa shida ya mazingira ni watu walio hatarini, yaani makundi maalum.

"Haki zilizoonekana kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi ni haki za kijamii kuanzia chakula, afya, elimu, upatikanaji wa majisafi na salama, kuishi katika mazingira stahiki na haki ya faragha ya familia," alisema.

Dk. Anna aliongeza kuwa haki za kiuchumi pia zimeendelea kuathiriwa na mabadiliko hayo hasa katika sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi na kwamba wananchi wanaendelea kuathirika zaidi kutokana na upatikanaji hafifu wa bidhaa za kilimo na uvuvi pamoja na kuwapo magonjwa mbalimbali yanayoathiri mifugo.

Kwa upande wa haki za kiutamaduni, mkurugenzi huyo alisema ripoti imebaini wananchi kuendelea kuhama maeneo yao ya asili kutokana na kukosa chakula na maji na kushindwa kufanya shughuli za kilimo ambazo ni tegemeo kwa ustawi wao.

"Makundi maalum kama vile wanawake na watoto, nao wameathiriwa kwani kwa kuhamahama, watoto wengi wameshindwa kufikia haki yao ya kupata elimu, wazazi wameendelea kutelekeza familia kutokana na kuhama kutafuta maeneo stahiki ya kuishi," alisema.

Dk. Anna alisema katika kutelekeza malengo ya maendeleo endelevu, LHRC inatoa wito kwa serikali, taasisi na jamii ya Watanzania kwa umoja wao kuchukua hatua za kuwezesha kutunza mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa manufaa ya vizazi vijavyo.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo (kulia) akiwa amesimama juu ya tangi la maji, akionyeshwa uharibifu uliofanywa na watu kukata misitu na kuharibu vyanzo vya maji katika Kijiji cha Naima, Kata ya Mbondo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwenge wa Uhuru wakagua kiwanda cha vioo cha Pwani

**Na Julieth Mkireri,**

MKURANGA

MWENGE wa Uhuru 2023 umekagua mradi wa ujenzi wa kiwanda cha vioo kinachojengwa katika Kijiji cha Mkiu, Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani kinachotarajiwa kuzalisha vioo tani 700 kwa siku.

Akitoa taarifa kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Abdallah Shaib, Meneja Biashara wa kiwanda hicho Xuehua Chen (SHARIFA), alisema mradi huo utakapokamilika utagharimu Sh. bilioni 500.

Xuehua alisema lengo la mradi huo ni kuhakikisha Tanzania inapunguza uagizaji wa vioo kutoka nje ya nchi, lakini pia kutekeleza kwa ufanisi sera ya uwekezaji wa viwanda ambayo imepewa kipaumbele na serikali.

Ujenzi wa mradi huo ulianza Julai 2022, uzalishaji wa bidhaa unatarajiwa kuanza Septemba 2023 na vioo vitauzwa ndani na nje ya nchi huku ajira za moja kwa moja 1,600 zitatolewa na zisizo za moja kwa moja 6,000.

Meneja huyo alisema kukamilika kwa mradi huo kutahamasisha uwapo wa huduma za kijamii ambazo zitachangia ukuzaji wa mji na uchumi wake.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge, alisema serikali imefanya mambo makubwa katika kuiinua sekta ya uwekezaji nchini na kwamba Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa akienda nje ya nchi kutafuta fursa za uwekezaji na matokeo yanaendelea kuonekana.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# DART uamuzi huu mtakuwa mmedhibiti wavunja sheria

**UAMUZI** wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), unaotarajia kuweka mageti maalum ya umeme kwenye njia za mabasi hayo kuzuia magari binafsi na bodaboda kupita njia hizo, utadhibiti madereva wanaopenda kuvunja sheria.

Mageti hayo tumeelezwa yatafungwa kifaa maalum kinachoweza kuhisi ambacho kitawezesha mageti kufunguka wakati mabasi yaendayo haraka yanapopita na kutofunguka yatakapopita magari ya watu binafsi na boda boda.

Uamuzi huu ikiwezekana ufanyike haraka ili kuwadhibiti wavunja sheria za barabarani.

Mwishoni mwa wiki, Kaimu Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa DART, Ng'wanashingi Gagaga, alitangaza uamuzi huo kupitia semina ya waandishi wa habari iliyofanyika mkoani Dodoma.

Mageti hayo kwa mujibu wa DART yatasaidia kwa kiwango kikubwa kuondoa ajali za mara kwa mara baina ya mabasi yaendayo haraka, magari binafsi na bodaboda zinazopita kwenye njia hizo. Mkataba kwa ajili ya kuanza kusimikwa kwa mageti hayo umeshasainiwa na mkandarasi atakayefanya kazi hiyo na kwa kuanzia yatatumika kwenye awamu ya kwanza ambayo ni njia ya Kimara-Kivukoni.

Mkataba uliowekwa ni wa wiki 32 kwa maana mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka huu inatarajiwa mageti yatakuwa yameshasimikwa na ile kero ya kupambana na wenye magari binafsi itakuwa imeondoka kwasababu hawataweza kupita tena kwenye njia hizo.

DART imeeleza kuwa kukosekana kwa mfumo huo kumesababisha watu wengi wakiwamo waendesha bodaboda kupita kwenye njia hizo na kusababisha usumbufu kwa mabasi yaendayo haraka na kuchelewesha safari zake.

Njia hizo zimetengenezwa maalumu kwa mabasi yanayoenda kwa haraka ili kuwapunguzia wananchi kukaa muda mrefu barabarani hali inayowachelewesha kufika kwenye sehemu zao za kazi.

Utaratibu huo wa kusimikwa mageti hautaruhusu mtu yeyote kupita isipokuwa mabasi yaendayo haraka pekee.

Kwa ilivyo sasa watu wamekuwa wakipita kwa ukaidi pamoja na DART kujitahidi kupambana nao na kufanya jitihada kubwa, lakini bado wanaendelea.

Baadhi ya jitihada zilizofanyika ni kuwashtaki kwa viongozi wao watumishi wa umma ambao wanalazimisha kupita kwenye njia hizo na wanachukuliwa hatua.

Baadhi ya watu imeelezwa hutumia njia hizo hata nyakati za mchana ambako hakuna msongamano wa magari na kusababisha usumbufu kwa magari yaendayo haraka na wakati mwingine kuchelewesha safari zake.

Kwa hakika hii inaondoa maana halisi ya kuwapo kwa njia hizo kwa magari maalumu yaliyotengewa kupita.


Kwanza watu hao wanaopita njia hizo wanaweza kusababisha ajali, ambazo zingine zimeshatokea na kuleta hasara kwa vyombo hivyo vya usafiri.

Watu wengine wametajwa kufanya mazoea ya kupita kwenye njia hizo kwasababu unaweza kukuta saa saba usiku anapita kwenye njia ya mwendokasi, wakati muda huo hauna msongamano. DART imehakikisha kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya kutumia njia za mabasi yaendayo haraka kwa kuwa wao ndiyo wanaongoza kufanya uhalifu huo wa kupita kwenye njia hizo.

Ni muhimu pia kuwafikia viongozi wao na kuwapa elimu hiyo ili angalau wapunguze matumizi ya njia hizo kwa sababu licha ya kupata ajali za mara kwa mara, lakini hawaachi kuzitumia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mafunzo vishikwambi hayakwepeki tena

Na Sabato Kasika

**MOJA** ya maombi ya walimu ambayo walitoa mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni, ni mafunzo ya matumizi ya vishikwambi walivyopewa na serikali ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

Vishikwambi hivyo viligawiwa kwa walimu wa ngazi zote wakiwamo wakufunzi wa vyuo ili vitumike kutimiza azma ya serikali ya kuhamasisha na kuboresha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ufundishaji na ujifunzaji.

Ilikuwa ni mwishoni mwa mwaka jana ndipo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alivigawa vishikwambi hivyo, lakini inaonekana wapo baadhi ya walimu ambao hawajapata mafunzo ya matumizi yake.

Hali hiyo ilidhihirisha katika kilele cha Mei Mosi mjini Morogoro, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi, walimu wanatoa ombi la mafunzo ya jinsi ya kuvitumia ili waweze kuboresha kazi yao ya kufundisha.

Ombi hilo linaonyesha wazi kuwa kuna uhitaji wa mafunzo hayo kwa vifaa hivyo vya TEHAMA, katika shule nchini hasa kwa walimu ili ufundishaji na ujifunzaji uweze uwe wa tija na kazi zisifanyike kwa mazoea.

Ninadhani ingekuwa vyema iwapo mafunzo hayo yataharakishwa kwa walimu wote wenye uhitaji, kwani inavyoonekena wapo baadhi yao hawajui matumizi yake, hivyo wangesaidiwa ili kufanikisha na kufikia lengo.

Lakini inashangaza, Waziri Mkuu Majaliwa, alishaiagiza Wizara za Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Sayansi na Teknolojia ya Habari kutoa mafunzo ya matumizi ya vishikwambi, hata hivyo, inaonekana hilo halijatekelezwa. Huenda kuna sababu na mojawapo ni masuala ya fedha.

Kitendo cha walimu kumwomba Rais wapewe mafunzo ya vifaa hivyo, kinaonyesha wazi kwamba maagizo ya Waziri Mkuu kwa Wizara Elimu, Ofisi TAMISEMI hayajafanyiwa kazi ipasavyo,

> **Ninadhani ingekuwa vyema iwapo mafunzo hayo yataharakishwa kwa walimu wote wenye uhitaji, kwani inavyoonekena wapo baadhi yao hawajui matumizi yake, hivyo wangesaidiwa ili kufanikisha na kufikia lengo.**

pengine baada ya Bunge la Bajeti, kazi itafanyika kwa vile bajeti itakuwa imeandaliwa.

Pamoja na hayo, ninaamini kwamba kwa hatua ya kugawa vishikwambi hivyo kwa walimu, ni hatua mojawapo ya kutaka kuimarisha TEHAMA kuanzia kwa walimu hadi kwa wanafunzi.

Vilevile mkakati wa serikali wa kutaka kujenga chuo cha kisasa cha TEHAMA eneo la Nala jijini Dodoma ili kuongeza kasi na ubunifu katika matumizi ya TEHAMA, ni wazi imedhamiria kusaidia vijana kuendeleza ubunifu wa jinsi wanavyoweza kuunda vifaa mbalimbali.

Hivyo, ingekuwa ni vyema iwapo kila upande utatimiza wajibu wake, hasa kwa wale walioelekezwa kutoa mafunzo kwa walimu ya jinsi ya kutumia vishishwambi ili nao wavitumie kufundishia wanafunzi.

Yapo baadhi ya maeneo ambayo tayari walimu wameshaanza kupata mafunzo hayo ikiwamo Halmashauri ya Mji wa Handeni mkoani Tanga ambayo walimu wake wameshanufaika.

Lakini kitendo cha walimu kujitokeza hadharani kwenye sherehe za Mei Mosi mbele ya Rais, kuomba mafunzo, kinaonyesha wapo wengi ambao hawajayapata na wanayahitaji.

Ninadhani ingekuwa vyema wale waliopewa jukumu la kutoa mafunzo ya matumizi ya vifaa hivyo wakafanya sehemu yao, ili ombi la walimu kuhusu mafunzo ya vishikwambi lisikike.

Taarifa inayotolewa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, wakati wa ugawaji wa vishikwambi hivyo, ni kwamba walimu wa shule za msingi za serikali 185,404, wa sekondari za umma 89,805, wathibiti ubora wa wilaya na kanda waligawiwa vishikwambi 1,666.

Wengine waliopata ni wakufunzi wa vyuo vya ualimu vishikwambi 1,353, wakufunzi wa vyuo vya maendeleo ya jamii 297, wa vyuo vya ufundi stadi 996, maofisa elimu mkoa, wilaya na kata 5,77 na Baraza la Mitihani Taifa 8,357.

# MUHAS yaja na kamati kumulika mitaala elimu ya juu, soko la ajira

**Na Gwamaka Alipipi**

CHUO Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) kimezindua kamati ya ushauri katika mitaala ili kuimarisha mazingira na mifumo ya kufundishia, kuhakikisha programu za mafunzo katika elimu ya juu zinaendana na mahitaji ya soko la ajira nchini.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kamati hiyo jana jijini Dar es Salaam, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, alisema pamoja na mambo mengine, wataalamu hao watatoa ushauri kuhusu mitaala ya kufundishia elimu ya msingi na sekondari.

"Kumekuwa na maswali mengi kuhusu ubora wa elimu yetu, wengine wamekuwa wakihoji kwanini wahitimu wetu hawaendani na soko la ajira? Hivyo, kamati hii itatoa ushauri katika masuala hayo," alisema Prof. Mdoe.

Alisema Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) utaboresha mitaala, rasilimali watu na mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vikuu na taasisi mbalimbali za elimu ya juu 23.

Alisema lengo kuu ni kuwezesha mfumo wa elimu ya juu ujikite katika kutoa elimu ujuzi ambayo itawawezesha wahitimu kuzalisha ajira au kujiajiri.

Prof. Mdoe alisema taasisi hizo ni vyuo vikuu vya umma 14, taasisi tatu zilizo chini ya wizara zinazosimamia elimu ya juu na taasisi tano za elimu ya juu zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Pia alisema mradi huo unakwenda kuanzisha kampasi 14 za vyuo vikuu katika mikoa ambayo ilikuwa haina taasisi za elimu ya juu kwa kujenga kampasi zitakazokuwa zinalelewa na vyuo vikuu kamili ambavyo vinatekeleza mradi huo.

"Kampasi hizo zitajengwa katika mikoa ya Mwanza, Kigoma, Lindi, Rukwa, Simiyu, Shinyanga, Tabora, Manyara, Ruvuma, Kagera, Katavi, Mara, Singida na Tanga, " alisema Prof. Mdoe.

Makamu Mkuu wa MUHAS, Prof. Andrea Pembe, alisema: "Kazi tutakazokwenda kuzifanya zitaleta uchumi ulio bora, tumekuwa tukichangia uchumi kupitia utoaji wa huduma bora ya afya."

Alisema kamati hiyo iliyoundwa imejumuisha wataalamu kutoka sekta ya waajiri binafsi, serikali, kampuni za dawa, wahitimu, wajasiriamali na wanafunzi.

# Msichana Initiative yataka waraka wa walioacha shule uwe kisheria

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Msichana Initiative kwa kushirikiana na wadau wengine wanaotetea wasichana, wameiomba serikali kuweka katika sheria waraka uliotolewa kwa ajili ya kuruhusu watoto wanaokatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo ujauzito, kurudi shuleni.

Waraka wa kuruhusu watoto kurudi shuleni ulitolewa na serikali Februari mwaka jana.

Akizungumza kwa niaba ya wadau hao, Mkurugenzi Mtendeji wa Msichana Initiative, Rebecca Gyumi, alisema wadau wanaona kuna haja waraka huo kuingizwa rasmi katika sheria, ili kuweka mwendelezo hata kwa viongozi wengine watakaokuja.

"Serikali ya awamu ya sita imefanya jambo zuri kuwarejesha watoto shuleni, wale wanaokatisha kwa sababu mbalimbali, lakini hatutaki uamuzi huu ukabaki katika waraka au mwongozo pekee.

"Tunataka uwekwe katika sheria ya elimu kwa sababu anaweza kuja kiongozi mwingine asiwe na mtazamo kama wa kiongozi aliyepo sasa, hivyo tukarudi tena tulikotoka," alisema.

Rebecca alisema kuna haja ya kuongeza nguvu kwa kushughulikia sababu zinazochangia mdondoko huo kwa wanafunzi.

"Hapa ndipo penye umuhimu zaidi kwa sababu kurudi shuleni ni mkakati umewekwa na serikali, lakini lazima kuangalia tunawezaje kushughulikia na kuongeza nguvu kupambana na sababu zinazochangia mdondoko huo.

"Mwaka jana Msichana Initiative tulifanya uchambuzi na kukutana na baadhi ya wasichana waliokatisha masomo kutoka kwenye vikundi 40 wilayani Nzega na Kongwa tukitaka kujua ni kwa kiasi gani wanaelewa fursa hiyo, tulibaini kwamba wapo ambao hawautambui kabisa mwongozo huo, ikiwamo wahusika wenyewe pamoja na wazazi wao.

"Na hata wale walioonekana kuufahamu kipaumbele chao kikubwa kilikuwa ni kutaka kurudi kwa mfumo rasmi, lakini wakitaka kujiendeleza na stadi za kazi ambazo zitawasaidia kujipatia kipato ili kujikimu kimaisha wao na familia zao.

"Na hata wazazi wengine wa wasichana hao waliowaona watoto wao kama tayari wameshakuwa watu wazima na tayari wana familia, wakihofu namna ya kutunza watoto endapo wasichana hao watarudi shuleni," alifafanua.

Gyumi alisema pamoja na serikali kuruhusu watoto hao kurejea shuleni, pia inatakiwa kuweka mazingira mazuri ambayo watakuwa huru kusoma bila kuwa na msongo wa mawazo juu ya namna gani watunze watoto wao baada ya kurejea shule.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

# MWITO WA KUTOA MAONI

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.**

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Vodacom Tanzania Limited, S.L.P 2369, Dodoma. | Kiwanja Na. 1 & 2, Kitalu "B", Dodoma. | Abel Kinyau (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta Matumizi Binafsi |
| 2. | MBT Muganyizi Investment, S.L.P 402, Dodoma. | Kiwanja Na. 78, Kitalu "C", Eneo la Mkombozi, Chamwino, Dodoma. | Edson Muganyizi (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya Kupikia ya LPG |
| 3. | Sungu Gas and General Supply, S.L.P 330, Dodoma. | Kiwanja Na. 29, Kitalu "H", Eneo la Kizota, Ndachi "B", Dodoma. | Fredrick Arbogast Chami (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya Kupikia ya LPG |
| 4. | GAPCO (T) Limited- Dodoma Service Station, S.L.P 9103, Dar es Salaam. | Mtaa wa Kuu, Dodoma. | Jean-Francois Schoepp (Raia wa Ubelgiji) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 5. | GAPCO (T) Ltd- Star Dodoma Service Station- Dodoma, S.L.P 9103, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.1 & 2, Kitalu "A", Mtaa wa Kuu, Dodoma. | Jean-Francois Schoepp (Raia wa Ubelgiji) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 6. | Puma Energy Tanzania Limited – Puma Dodoma Service Station, S.L.P 9043, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "94", Eneo la Chinangali, Dodoma. | Fatma Abdallah (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 7. | Felister Emanuel Tesha T/A Faidia Service Station, S.L.P 119, Mafinga. | Kiwanja Na.163, Kitalu "A", Kijiji cha Bandabichi, Iringa. | Felister Emanuel Tesha (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 8. | Ngumbi Services and Company Limited, S.L.P 281, Mafinga. | Kijiji cha Usokami, Mufindi, Iringa. | Christian Frances Ngumbi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 9. | Shemsa Mohamed Sharji, S.L.P 1082, Iringa. | Kiwanja Na.15, Kitalu "15", Iringa. | Shemsa Mohamed (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya Kupikia ya LPG |
| 10. | Asha hamud Salum T/A Mars Petrol Station, S.L.P 42, Nzega | Eneo la Kitangili, Nzega, Tabora. | Asha Hamoud Salum (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 11. | FAB International Limited, S.L.P 70419, Dar es Salaam | Eneo la kijiji cha Rungwa, Manyoni, Singida. | Farid Ahmed Bazar (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 12. | Yesseh P. Kimonga Petrol Station, S.L.P 81, Kiomboi. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "J", Old Kiomboi, Iramba, Singida. | Yesseh Peter Kimonga (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 13. | Mwanjalis Oil Company Limited, S.L.P 132. Tunduma. | Kiwanja Na. 50, Kitalu "K", Mpemba, Tunduma, Momba, Songwe. | Japhary Roman Mwampuwa (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 14. | Selestin Benedict Mhagama – Govidet Negelo & Company, S.L.P 40556, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 700, Kitalu "Y", Mjimwema, Njombe, Njombe. | Selestin Benedict Mhagama (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 15. | Olympic Petroleum (T) Limited – Iwambi Petrol Station S.L.P. 16484 Dar es Salaam | Kiwanja Na. 1099, Kitalu "F", Eneo la Iwambi, Mbeya. | Ally Adon (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 16. | Kyimo Filling Station-Goye S.L.P. 247 Tukuyu | Kijiji cha Goye, Rungwe, Mbeya. | Huruma Paul Malundi (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 17. | TSN Oil (T) Ltd – Ruangwa Filling Station, S.L.P 12288, Dar es salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu H, Eneo la Kilimahewa, Ruangwa, Lindi. | Ahmed Mohamed Baghozah (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 18. | Ester Malinyi Filling Station, S.L.P 67315, Dar es Salaam. | Eneo la Mwembeni, Kata ya Mlinyi, Ulanga, Morogoro. | Augustino Alphonce Ngowi. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 19. | Easter Filling Station Mbingu- Kilombero, S.L.P. 67315, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. MBG/SQ/010, Eneo la Mbingu, Kilombero, Morogoro. | Augustino Ngowi. (Mtanzania). | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 20. | Afroil Investment Limited, S.L.P. 38383, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 172, Kitalu "E", Eneo la Msamvu, Morogoro. | Hilmi Ahmed Mbaraka (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 21. | Sim Oil Limited, S.L.P 9150, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 410, Kitalu Na. "4", Eneo la Habour view Towers- Samora Avenue, Ilala, Dar es Salaam. | Fatima Mahsen Rashid. (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya Mafuta |
| 22. | Davida Oil Limited, S.L.P 40258, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 54, Kitalu "7", Eneo la Mwanagati, Ilala, Dar es Salaam. | Julius Mwita Makere (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 23. | Kobil Tanzania Ltd-Ferry Service Station, S.L.P 32570, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 68, Kitalu "A", Kigamboni, Dar es Salaam. | Davis E. Mosha (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 24. | Oryx kimara ss, S.L.P 9540, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 584, Kitalu "A", Eneo la Kimara Matangini, Ubungo, Dar es Salaam. | Kalpesh Mehta. (Raia wa Uingereza) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 25. | Sovavi Oil- Kinyerezi, S.L.P 11702, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1633, Kitalu "A", Eneo la Kinyerezi, Ilala, Dar es Salaam. | Elinisafi E. Lukenga. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 26. | A. S. Company ltd – Gongo la mboto filling station, S.L.P 15711, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2003, Kitalu "E", Eneo la Gongo la Mboto, Ilala, Dar es Salaam. | Faraj Ally Saeed (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 27. | New Msimbazi Kerosene Co. Ltd- Temeke, S.L.P 21531, Dar es Salaam. | Eneo la Mpolwe, Temeke, Dar es Salaam. | Mohamed Bahashwan (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 28. | Davida Oil Limited, S.L.P 40258, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 54, Kitalu "7", Eneo la Mwanagati, Ilala, Dar es Salaam | Julius Mwita Makere (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 29. | Kobil Tanzania Ltd-Ferry Service Station, S.L.P 32570, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.68, Kitalu "A", Kigamboni, Dar es Salaam. | Davis E. Mosha (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 30. | Uchira Gas Supply, S.L.P 304, Mtwara. | Kiwanja Na. 4, Eneo la vigaeni, Mtwara. | Emmanuel Roman (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya Kupikia ya LPG. |
| 31. | Mwanza Gaz Limited, S.L.P 5142, Mwanza | Kiwanja Na. 3&4, Kitalu "L", Eneo la Usagara, Misungwi, Mwanza. | Mukhtar Ahmed (Mnyarwanda) | Leseni ya Jumla ya Gesi ya Kupikia ya LPG |
| 32. | GBP Tanzania Limited, S.L.P 3728, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.45, Kitalu "M", Eneo la Kiseke (Pasiansi Low Density), Ilemela, Mwanza. | Badar Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 33. | Emmanuel Yeroboam Silaa, S.L.P 362, Geita. | Kijiji cha Ntinachi, Nyamilimilwa, Geita | Emmanuel Yeroboam Silaa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 34. | GBP Tanzania Limited, S.L.P 3728, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.1, Kitalu "C", Eneo la Muungano, Chato, Geita. | Badar Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 35. | Mathayo Sitta Budeba, S.L.P 56, Kahama. | Kiwanja Na.2617, Kitalu "R", Eneo la Mbulu, Kahama, Shinyanga. | Mathayo Sitta Budeba (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 36. | Ryoba Tindo Wambura T/A Tindo Filling Station, S.L.P. 68, Tarime. | Kijiji cha Nyangoto, Tarime, Mara. | Ryoba Tindo Wambura (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

# RC awaonya watendaji kamisheni ya asilimia 10

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amekemea vitendo vinavyofanywa na baadhi ya watendaji katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida wanaoagiza nje ya mkoa vifaa vya ujenzi wa miradi ya shule ili kupata kamisheni, maarufu asilimia 10.

Alikemea tabia hiyo juzi baada ya kutembelea miradi ya ujenzi wa shule inayotekelezwa katika manispaa hiyo kwa fedha za Mradi wa Kuboresha Upatikanaji wa Fursa Sawa katika Ujifunzaji Bora kwa Elimu ya Awali na Msingi Tanzania Bara (BOOST).

"Maelekezo ya miradi ya BOOST yalikuwa ni kwamba vifaa vya ujenzi vinunuliwe karibu na maeneo ya mradi unapotekelezwa. Sasa kwanini manispaa katika mradi huu wa ujenzi wa Shule mpya ya Msingi ya Nyerere mmeagiza nondo Dar es Salaam? Ninajua mnafanya haya kwa ajili ya 10 percent (asilimia 10). Mpate chochote," alisema.

Serukamba alisema kuagiza vifaa nje ya mkoa wakati vinapatikana ndani ya Mkoa wa Singida kuna uwezekano mkubwa wa kuchelewa kuletwa na hivyo kuchelewesha kuanza ujenzi, jambo ambalo limeanza kujionyesha katika Manispaa ya Singida.

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Paskas Mragili, alisema inashangaza kuona nondo zilizopo katika maduka ya vifaa vya ujenzi mjini Singida ambazo Manispaa ya Singida wanasema hazifai na kuamua kuagiza Dar es Salaam ndizo hizo ambazo zinatumika kujengwa maghorofa Singida.

Kufuatia kauli hiyo, Mkuu wa Mkoa Singida alisema watendaji wa Manispaa ya Singida kama waliona hivyo vifaa wanavyohitaji katika ujenzi havipo, walipaswa kurudi mezani kujadiliana badala ya kuamua kuagiza Dar es Salaam na hivyo kukiuka maelekezo ya utekelezaji wa miradi ya BOOST.

Meya wa Manispaa hiyo, Yagi Kiaratu, alisema wamepokea maelekezo ya Mkuu wa Mkoa na kumhakikishia watakaa kujadilia suala hilo ili miradi iliyopangwa ikamilike kwa wakati.

Hivi karibuni serikali kwa kushirikiana na wafadhili iliupatia Mkoa wa Singida Sh. bilioni 9.024 kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

Fedha hizo ambazo ni maalum kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule yakiwamo madarasa, vyoo na madawati, mgawanyo wake ni: Wilaya ya Ikungi Sh. bilioni 1.47, Iramba Sh. bilioni 1.59, Itigi Sh. bilioni 1.39, Manyoni Sh. milioni 909, Mkalama Sh. milioni 925, Singida DC Sh. bilioni 1.351 na Manispaa ya Singida Sh. bilioni 1.371.



Mkuu wa Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Goodluck Mlinga (katikati), akishirikiana na wananchi kufyatua matofali juzi, kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Msingi Mbonde iliyopo Kata ya Nangando. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## NBC yatambulisha huduma yake mpya Kanda ya Ziwa

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imeitambulisha rasmi huduma yake mpya ya kidigitali inayofahamika kama 'NBC Connect' kwa wateja wake wa Kanda ya Ziwa.

Huduma hiyo inalenga kuunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha mfumo jumuishi wa utoaji na upatikanaji wa huduma za kifedha nchini (financial inclusion) kupitia huduma zake zilizorahisishwa.

Utambulisho wa huduma hiyo katika mikoa ya Kanda ya Ziwa ya Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga, Simiyu na Geita ni mwendelezo wa jitihada za benki hiyo kuisogeza karibu zaidi huduma hiyo kwa wateja wake kufuatia uzinduzi wake uliofanyika jijini Mbeya hivi karibuni.

Hafla ya utambulisho wa huduma hiyo Kanda ya Ziwa ilifanyika jijini Mwanza mwishoni mwa wiki, ikihudhuriwa na wadau mbalimbali wa benki, viongozi wa serikali, wateja na maofisa wa benki hiyo.

Mkuu wa Kitengo cha Wateja wa Kimataifa wa Benki ya NBC, Wilson Nkuzi, alisema huduma hiyo ni mwendelezo wa jitihada za benki hiyo katika kuwapatia watu wake huduma bora za kibenki zilizorahisishwa, za uhakika, salama na zinazoendana na mahitaji ya wateja.

"Kupitia huduma hii, sasa kampuni pamoja na taasisi mbalimbali ambazo ni wateja wa NBC hapa Kanda ya Ziwa wanaweza kupata uzoefu mpya wa huduma za kibenki kupitia huduma ya NBC Connect, ikiwa ni ingizo jipya la huduma za kibunifu za kidigitali. NBC Connect inawahakikishia wateja wetu huduma salama, sehemu yoyote na muda wowote kwa njia ya mtandao," alisema.

Kwa mujibu wa Nkuzi, kupitia huduma hiyo wateja wa benki hiyo wana uwezo wa kutumia simu zao au kompyuta kufanya miamala kwa urahisi zaidi ikiwamo malipo ya ndani na nje ya nchi na malipo ya serikali kwa mkupuo mmoja bila kutumia muda mrefu.

Katika hafla hiyo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Bulandya Elikana, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, aliishukuru Benki ya NBC kwa ubunifu huo mzuri na wenye tija katika urahisishaji wa huduma za kifedha nchini. Aliwahimiza wateja wa benki hiyo na jamii kutumia mfumo huo mpya wa kibenki ili kurahisisha shughuli zao za kila siku.

"Kama mkoa na serikali ambao pia ni wateja wa Benki ya NBC, tunaamini kwamba ujio wa NBC Connect mbali na kuunga mkono jitihada za serikali katika kuvutia wananchi wengi kutumia huduma rasmi za kibenki, pia utatasaidia sisi kama wateja wa benki hii kufanya miamala ya kibenki kwa urahisi zaidi hasa ikizingatiwa kuna malipo mengi ya serikali yanayofanyika kupitia benki hii. Tunawashukuru sana na zaidi tunawapongeza kwa ubunifu huu," alisema.

# DART kuweka mageti ya umeme vituoni kuzuia bodaboda, magari

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) unatarajia kuweka mageti maalum ya umeme katika njia za mabasi hayo kwa ajili ya kuzuia magari binafsi na bodaboda kupita njia hizo.

Mageti hayo yatafungwa kifaa maalum (sensor) ambacho kitawezesha mageti kufunguka tu wakati mabasi yaendayo haraka yanapopita na kutofunguka yatakapopita magari ya watu binafsi na bodaboda.

Mwishoni mwa wiki, Kaimu Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa DART, Ng'wanashingi Gagaga, alibainisha hayo wakati wa semina ya waandishi wa habari mkoani Dodoma.

Alisema uamuzi huo utasaidia kwa kiwango kikubwa kuondoa ajali za mara kwa mara baina ya mabasi yaendayo haraka, magari binafsi na bodaboda zinazopita katika njia hizo.

Alisema wameshatia saini mkataba na mkandarasi kwa ajili ya kuanza kusimika mageti hayo na kwa kuanzia yatatumika katika awamu ya kwanza ya mradi huo ambayo ni njia ya Kimara-Kivukoni.

"Mkataba ni wa wiki 32 kwa maana mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka huu tunatarajia mageti yatakuwa yameshasimikwa na tutakuwa tumeondokana na kero ya kupambana na wenye magari binafsi kwa sababu hawatoweza kupita tena kwenye njia hizo," alisema.

Gagaga alisema kukosekana kwa mfumo huo kumesababisha watu wengi wakiwamo waendesha bodaboda kupita kwenye njia hizo na kusababisha usumbufu kwa mabasi yaendayo haraka na hata kuchelewesha safari zake.

"Kwenye hizi njia hakuna mtu yeyote anayeruhusiwa kupita isipokuwa mabasi yaendayo haraka. Watu wamekuwa wakipita kwa ukaidi tu na tumejitahidi kupambana nao. Tumefanya jitihada kubwa lakini bado, ingawa wamepungua," alisema.

Alitaja baadhi ya jitihada walizofanya ni pamoja na kuwashtaki kwa viongozi wao watumishi wa umma ambao wamekuwa wakilazimisha kupita kwenye njia hizo na wamekuwa wakichukuliwa hatua.

Alisema kuna baadhi ya watu ambao wamekuwa wakitumia njia hizo hata nyakati za mchana ambako hakuna msongamano wa magari, hivyo kusababisha usumbufu kwa magari yaendayo haraka na wakati mwingine kuchelewesha safari zake.

"Watu wengine wamefanya mazoea tu ya kupita kwenye njia hizi kwa sababu kuna mtu unaweza kukuta saa saba usiku anapita kwenye njia ya mwendokasi, sasa saa nane usiku kuna msongamano wa magari kweli? Kwa hiyo, mageti haya yatakuwa suluhisho kwa sababu wakipita hayatofunguka," alisema.

Aliongeza kuwa wataendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya kutumia njia za mabasi yaendayo haraka kwa kuwa wao ndio wanaongoza kufanya uhalifu huo wa kupita katika njia hizo.

Alisema watajitahidi kuwafikia viongozi wao na kuwapa elimu hiyo ili angalau wapunguze matumizi ya njia hizo. Wamekuwa wanapata ajali za mara kwa mara lakini hawaachi kuzitumia.

## Kilio cha Mbunge ufuatiliaji ujenzi barabara chazaa matunda

**Na Jaliwason Jasson,** MBULU

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, amesema kutokana na Mbunge wa Mbulu Vijijini, Flatei Masaay, kuvalia nguja suala la ujenzi wa barabara ya Labay-Haydom kwa kiwango cha lami ilimlazimu kuwaagiza watendaji wa wizara hiyo, kutomruhusu mbunge huyo, kuingia kwenye ofisi zao kufuatilia jambo hilo.

Naibu Waziri huyo, alisema hayo jana wakati wa utiaji saini mkataba wa ujenzi wa barabara ya Labay-Haydom kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 25 ambayo itajengwa na mkandarasi wa Kampuni ya Jiangxi geo engineering corporation Group.

"Ilifika mahali ukimuona Flatei anakuja ofisini nawaambia wasaidizi wangu mwambie hayupo kwa kuwa kila aliposimama Bungeni alizungumzia barabara hii," alisema Kasekenya.

Aidha, alisema kelele za mbunge huyo hazikuishia wizara ya ujenzi tu bali zilikuwa zinamfikia Rais Samia Suluhu Hassan, ndiyo maana fedha ikatolewa na serikali ili barabara ijengwe.

Alisema Mkoa wa Manyara una mtandao mdogo wa barabara za kiwango cha lami na kuondoa uchache wa barabara za lami mkoani humo zitajengwa kubwa tatu za kitaifa.

Vilevile, aliwaomba wananchi kulinda barabara zitakazojengwa kwa kuwa kwa ujenzi wa barabara una gharimu fedha nyingi.

"Wakala wa Barabara (TANROADS), hakikisheni thamani ya barabara inaonekana na kipaumbele cha ajira kiwe kwa wananchi wa Mbulu sio watu kutoka mbali," alisema.

Alitoa onyo watu wenye tabia ya kuiba mafuta na vifaa vingine vya ujenzi kuacha, kwa kuwa hawamkomoi mkandarasi au Rais bali ni kulisababishia taifa hasara.

Awali, akitoa taarifa ya ujenzi wa barabara hiyo, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Rogatus Mativila, alisema ujenzi wa barabara hiyo utagharimu Sh. bilioni 42.271 na utafanyika kwa miezi 18.

Alisema barabara ya mchepuo ya Serengeti (Bypass), yenye kilometa 389 kwa Mkoa wa Manyara ziko kilometa 113 na hiyo ni awamu ya pili ambayo inakamilisha kilometa 50 zilizotanguliwa na barabara ya Garbab/ Mbulu yenye kilometa 25.

Naye Mbunge wa Mbulu Vijijini, Flatei Masaay, aliomba msamaha kwa kupiga sarakasi bungeni kwa kudai barabara.

Masaay, alisema hatazuia bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka 2023/24 itakayosomwa wiki hii.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, alisema mkoa huo una tatizo la kuunganisha barabara za mkoa.

# Wamwomba Samia kuingilia kati wananchi kuhamishwa

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

ZAIDI ya wananchi 4,000 wa jamii ya kifugaji ya Kimasai kutoka Kijiji cha Kimotorok, Kata ya Loibosiret, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wamemwomba Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuingilia kati suala la wananchi kutakiwa kuondoka katika eneo hilo na kuhamia Wilaya ya Kondoa mkoani Manyara.

Eneo la kijiji hicho, lina ukubwa wa kilomita za mraba 1,000 na linapakana na pori tengefu la Mkungunero na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana kwa niaba ya wananchi wa kijiji hicho, Yohana Parmelo, alisema hadi sasa ameishi katika eneo hilo kwa kipindi cha zaidi ya miaka 40 na hapo ndipo chimbuko la kizazi chao.

"Tumeandamana tukiwa tumebeba mabango ya kupinga kitendo hiki tunachofanyiwa kwa kuwa tunatakiwa kutoka kwenye ardhi yetu kwa kuwa tumeelezwa kuwa siku sio nyingi eneo hili litamegwa na kuingizwa Kondoa kutoka Wilaya ya Simanjiro.

"Sisi ni jamii ya kifugaji ukituambia tuhamie Kondoa sijui tutakwenda kuishi vipi kwa kuwa tuna ng'ombe wengi na kule hakuna maeneo makubwa ya kufugia na wenzetu ni wakulima na wafanyabiashara," alisema.

Alifikisha kilio chake kwa Rais Samia Suluhu Hassan, akimwaomba awahurumie waruhusiwe kubaki hapo na waendelee na shughuli zao za ufugaji na uhifadhi wa mazingira.

Naye Lukas Ndutui, alisema malalamiko yao yametokana baada ya kuelezwa wanatakiwa kuondoka kwa kuwa eneo hilo ni la hifadhi na liko wilaya nyingine ya Kondoa.

"Naomba Rais Samia kwa kuwa ni mama mwenye watoto atutendee huruma yake kwa kuwa katika gazeti la serikali la mwaka 1966 vitongoji vyote vya Tanzania na mikapa yake viliorodheshwa kikiwamo hiki cha kwetu hivyo kwa sasa tunashangaa wanatuambia tuhame kwa kuwa kijiji kiko Kondoa.

"Mimi ni mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakati wa uongozi wa Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, niliwahi kuwapeleka Ikulu viongozi wa mila (Malaigwanani), tulimweleza jambo hili anafahamu hilo, hivyo hatujui kwa nini mambo yamebadilika," alisema.

Happynes Taitas, alisema wananchi wana huzuni, wananyanyasika kwa kuwa wamezaliwa kijijini hapo, lakini wanatakiwa kuhama kwenda sehemu nyingine.

Akijibu malalamiko hayo kwa njia ya simu, Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Dk. Hamisi Mkanachi, alisema kuna vikao vimefanyika kwa viongozi wa pande mbili za mkoa wa Dodoma na Manyara kutafuta suluhu ya mgogoro huo.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera, alisema jambo hilo liko serikalini ngazi ya mkoa na linafanyiwa kazi na suala hilo bado halijakamilika.

"Bado Kimotorok iko Simanjiro, sasa mimi kama DC nina peperusha bendera na wanaona ninapopita hapo kwa nini watoe malalamiko hayo ilhali jambo halijakamilika kwa kuwa serikali ina utaratibu wake.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Utalii ya Origin Trails, Emmanuel Motta (kulia), akitoa maelekezo kuhusu namna ya kupanda Mlima Kilimanjaro kwa usalama kwa baadhi ya wageni kutoka nchi mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) mjini Moshi mwishoni mwa wiki, kabla ya kuupanda kuadhimisha miaka 60 ya Umoja wa Afrika (AU). **PICHA: JAMES LANKA**

# IJA yajisifu kutoa wanafunzi mahiri wa sheria

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

CHUO cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), kimejinasibu kwa kuzalisha wanafunzi mahiri wa sheria, ambao wamekuwa na tija kubwa nchini katika kada ya utoaji haki.

Mhadhiri Msaidizi wa Chuo cha IJA, Tundonde Mwihomeke, akizungumza katika banda la chuo hicho, kwenye maonyesho ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) yaliyofanyika jijini Arusha, alisema ufundishaji kwa njia ya mfumo mahiri umesababisha wanafunzi wao kuwa na ujuzi na utendaji kazi mzuri kwenye mafunzo kwa vitendo mahakamani.

"Chuo chetu kinawafundisha wanafunzi mitaala ya kisasa ya umahiri tunahakikisha tunamfundisha darasani na tunampeleka mahakamani ili kupata ujuzi wa kivitendo na hii imetusaidia sana chuo chetu kuzalisha wanafunzi bora," alisema Tundonde.

Vilevile, wanafunzi wanaomaliza chuoni hapo, wamekuwa wakifanya vizuri wanapokwenda ngazi za juu za elimu ya sheria, akitoa mfano wa mwanafunzi bora wa Mzumbe ngazi ya shahada mwaka jana kuwa alitokea IJA.

Tundonde alisema chuo hicho, kinaendelea kupitia miongozo yake ya ufundishaji ili mwanafunzi aendane na soko la sasa la sheria na aweze kujiajiri na kuajiriwa.


"IJA huwa na kawaida ya kupitia miongozo yake ya ufundishaji, lengo ni kumfanya mwanafunzi wetu amalize na kufaa soko la ajira na kujiajiri mwenyewe," alisema Tundonde. Chuo cha IJA (Institute of Judicial Administration), kinatoa mafunzo ya sheria kwa ngazi ya stashahada na astashahada, kadhalika kinafanya utafiti wa kisheria na mafunzo kwa wadau wanaojihusisha na masuala ya haki na sheria.

Ofisa Udahili wa Chuo cha IJA, Magdalena Mlumbe, alisema chuo kina miundombinu muhimu na ya kisasa, ikiwamo maktaba, ambayo ina vitabu muhimu katika maarifa ya sheria.

"Chuo chetu kina miundombinu ya kisasa ambayo ni muhimu katika ufundishaji, mathalani kuna maktaba ya kisasa yenye vitabu vya sheria, ambavyo si rahisi kuvipata kwenye maktaba zingine," alisema Magdalena.

Magdalena aliongeza kuwa chuo kina miundombinu yote muhimu, ikiwamo huduma ya malazi, zanahati na viwanja vya michezo.

Ahmed Shemle, mhitimu wa zamani wa chuo cha IJA, alisema elimu ya sheria aliyoipata kutoka chuoni hapo, imemsaidia kwenye masuala mbalimbali.



# Wavuvi waomba mashine kuanika, kukaushia dagaa

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

BAADHI ya wavuvi wa mwalo wa dagaa Nyamkazi uliopo Kata ya Miembeni, Manispaa ya Bukoba, mkoani Kagera wameiomba serikali kuwasaidia upatikanaji wa mashine za kuanikia na kukausha dagaa hususani katika msimu wa masika ili kudhibiti hasara.

Wakizungumza na Nipashe jana katika mwalo huo, wavuvi hao pamoja na wachuuzi wa dagaa walisema biashara hiyo inakuwa ngumu kipindi cha mvua kutokana na kutegemea mionzi ya jua kukausha dagaa wao baada ya kutoka ziwani na kuomba msaada wa mashine za kukaushia.

"Hali hii inafanya kushuka kwa mapato ya wavuvi kutokana na dagaa kuharibika wakati mwingine kuuzwa kwa bei ya hasara ili waishe, lakini tungelikuwa na mashine wangekaushwa na kuuzwa kwa bei rafiki na kufanya biashara hii kuongeza pato la taifa," alisema Shaidu Mshemba, mvuvi.

Aneth Anatory, mnunuzi wa dagaa mwalo wa Nyamkazi alisema, upatikanaji wa dagaa kwa sasa ni mzuri, lakini tatizo kubwa ni jinsi ya kukausha dagaa hao kutokana na kukosa sehemu ya uhakika zaidi ya kutegemea jua ambalo kwa kipindi cha masika linawaka kwa shida. "Zikiwapo mashine hizo hata kwa kuzikodi au kukopeshwa itatubidi tugharamikie maana unakuta mtu amenunua ndoo saba hadi kumi ambazo kwa ndoo moja inauzwa Sh. 25,000 katika msimu wa kiangazi, lakini kwa masika ndoo hiyo hiyo inakuwa Sh.10,000, lakini anaingia hasara kubwa pale jua lisipowaka," alisisitiza Aneth.

Mwenyekiti wa ulinzi na usimamizi raslimali za wavuvi mwalo wa Nyamkazi alisema, tayari wamepokea ombi hilo kutoka kwa wavuvi na wachuuzi wa dagaa na limefikishwa serikalini kwa utekelezaji.

Ofisa Uvuvi Mkoa wa Kagera, Efrahim Mkama, alisema, ili kusaidia wavuvi hao ni kuwapa elimu ya ushirikiano baina yao na taasisi za kifedha mkoani humo ili wapatiwe mikopo itakayowawezesha kununua mashine hizo na kuzimiliki wenyewe.

Alisema zipo kampuni zinazotengeneza mashine ikiwamo (SIDO) zenye uwezo wa mitambo hiyo na kupeleka kwenye maeneo yao ya kuanikia dagaa, ni suala la wao kununua na serikali imewapatia tayari maeneo ya kuanikia dagaa wao.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, akimbeba mtoto alipotembelea wodi ya wazazi katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga na kuwajulia hali ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Siku ya Wauguzi kiwilaya juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# TANROADS kuendeleza barabara za lami zilizopandishwa hadhi

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mkoa wa Shinyanga, umeanza matengenezo ya barabara zilizopandishwa hadhi na serikali kuu kuwa za TANROADS zenye urefu wa kilomita 171.26 kutoka Masumbwe mkoani Geita, kuelekea Halmashauri ya Ushetu pamoja na Mwambomba hadi Ulowa, mkoani Shinyanga.

Akizungumza juzi wakati wa ukaguzi wa ujenzi wa barabara ya Mwambomba-Ulowa yenye urefu wa kilomita 65.87, Meneja wa TANROADS Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Mibara Ndirimbi, alisema baada ya barabara hizo kupandishwa hadhi kutoka TARURA tayari utekelezaji wake umeanza ili kuunganisha mikoa ya Geita na Shinyanga.

"Zimepandishwa hadhi katika mwaka wa fedha 2021/22 na matengenezo yake yanaendelea kupitia fedha kutoka serikali kuu, lengo likiwa ni kuhakikisha mikoa hii inaunganishwa na kuongeza kasi ya uchumi," alisema.

Aidha, aliishukuru Wizara ya Ujenzi pamoja na Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Rogatus Mativila kwa maelekezo anayotoa ya namna bora ya utengenezaji wa barabara hizo.

Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema barabara zinazounganisha mikoa hiyo zinafungua uchumi na kuboresha hali ya usafiri kwa wananchi na usafirishaji wa malighafi za viwandani na mazao kutoka mashambani kwenda kwenye masoko.

Baadhi ya wananchi wa Kata ya Bugomba A, walisema ujenzi wa barabara hizo utawasaidia kuondoa adha ya usafiri na usafirishaji hususani katika kipindi cha mvua.

"Awali barabara zilikuwa zimeharibiwa na mvua inayoendelea kunyesha, kwa sasa matengenezo yamesaidia zinapitika na zinatuwezesha kupeleka mazao kwenye masoko badala ya kuuza kwa walanguzi wanaotumia vipimo vya lumbesa," alisema Raheli Thumuni.

# Bandari iliyofungwa miaka 21 yafunguliwa Chato

**Na Daniel Limbe,** CHATO

BANDARI ya Nyamirembe, wilayani Chato, mkoani Geita iliyofungwa kwa zaidi ya miaka 20 imefunguliwa na kuanza shughuli za usafiri na usafirishaji mizigo ndani na nje ya nchi huku wafanyabiashara kutoka nchi wanachama wa Afrika Mashariki (EAC), wakialikwa kutumia bandari hiyo kusafirisha mizigo yao kwa gharama nafuu na kwa haraka.

Bandari hiyo ilisimama kufanya kazi mwaka 2002, mwaka 2017/18 serikali kupitia TPA ilitenga Sh. bilioni 4.1 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi mkubwa wa bandari hiyo na mkandarasi alianza kazi 2018 na kukamilisha 2019, licha ya kukamilika haikuendelea kutumika.

Akizungumza na wananchi bandarini hapo, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela, alisema serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Nchini (TPA), imetangaza ahueni kwa mizigo itakayohifadhiwa kwenye bandari hiyo kutoka siku saba za awali hadi siku 30 ili kuwavutia wafanyabiashara wengi.

Kadhalika alieleza kuwa kuzinduliwa kwa bandari hiyo ni maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye anatamani kuona ushirikiano wa kibiashara wa nchi wanachama unaimarika kupitia bandari hiyo huku akiwataka wafanyabiashara wakubwa wa ndani ya nchi kuchangamkia fursa za kibiashara kwa lengo la kukuza uchumi binafsi na taifa.

Vilevile, meli kubwa zinazotoa huduma ndani ya Ziwa Victoria, zitafanya safari zake kupitia Bandari ya Nyamirembe ili kuinua uchumi wa Mkoa wa Geita huku akiwataka wananchi kuendelea kuzalisha mazao kwa wingi ili kujipatia kipato.

Mkuu wa Wilaya ya Chato, Deusdedith Katwale, alisema kurejeshwa kwa huduma hiyo kutasaidia kuinua uchumi wa wananchi katika maeneo ya Chato, Biharamulo, Ngara, Muleba na nchi jirani za Rwanda, Burundi na Uganda.

Awali, Mkuu wa Idara ya Utekelezaji TPA Ziwa Victoria, Fransisco Mwanga, alisema eneo la bandari hiyo lilipimwa tangu mwaka 1954 likiwa na ukubwa wa ekari 126 na kwa kipindi cha miaka ya 1880 hadi mwaka 1990 bandari hiyo ilikuwa ikihudumia meli ya Mv Serengeti, Mv Liemba, Mv Ukerewe na Mv Klarias kwa kusafirisha abiria na mizigo katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria.

Mwanga alisema jitihada za kuongea na wenye meli zinafanyika ili kurejesha safari za Bandari ya Nyamirembe ikiwa ni pamoja na kutoa ahueni ya kutunza mizigo bure kutoka siku saba hadi siku 30.

Nipashe
# TESA
Jumanne Mei 23, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 12


Mgomo Kariakoo ulivyoibua ari ya kukutana na Waziri Mkuu



Ukurasa 13

Masharti na kukosa mbinu utafutaji kunavyowakwamisha wenye ulemavu

Ukurasa 14



## Zinaibuliwa mbinu kurejesha wasiopenda shule darasani

ELIMU

**NA MARCO MADUHU, SHINYANGA**

# Mwanandoa hili ni somo mikopo umiza, komaa usifilisiwe, simama na sheria



Wanafamilia wanaweza kulala nje baada ya nyumba kutwaliwa na watoa mikopo umiza. **PICHA: MTANDAO**

KINAMAMA kukopa kwenye taasisi za ukopeshaji pengine bila kuwa na elimu au ufahamu wa kile kitakachowapata watakapokwama kulipa imekuwa chanzo cha mizozo na migogoro kwenye familia.

Fedha hizo zikibatizwa mikopo umiza au kausha damu, licha ya kuchochea migogoro ya kifamilia na kuvunja ndoa kuna wakati inaelezwa kusababisha vifo kwa vile wakopaji hujitia kitanzi.

Wakati umefika jamii kuelimishwa ili kufahamu kuwa kukopa mkopo wowote uwe umiza au wa kikundi na kuweka rehani mali za familia bila taarifa kwa mkeo au mumeo, iwapo una ndoa ni hatia na ni kinyume cha sheria, kwa vile wanandoa wanatakiwa kuwa na ridhaa.

Anasema Mwanasheria wa Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT), Teresia Fabiani, akirejea Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, inayosema mwanamke au mwanaume akienda kukopa bila makubaliano ya upande mmoja mkopo huo ni batili na mali haipaswi kuchukuliwa sababu mkataba hauna makubaliano ya pande mbili.

Anaeleza kuwa Sheria ya Mikopo inayohusiana na kuweka mali rehani ya mwaka 2008 nayo inasema mkopaji anapaswa kusema ukweli kama ana mke au mume na kutoa nyaraka ya cheti cha ndoa na pia mkopeshaji ana wajibu wa kuchunguza ukweli wa taarifa alizopewa.

Anasema sheria hiyo inasema mkopaji akitoa nyaraka za uongo anafungwa kifungo cha miezi 12, hivyo mkopaji anapaswa kutoa taarifa za ukweli ili kukwepa adhabu hiyo, na pia kama ameficha kuonyesha kama ameolewa na akapata mkopo, utakuwa batili.

"Kama ameolewa au kuoa wakati akikopa kisheria ni lazima ridhaa ya mume au mke itolewe kuweka rehani mali kabla ya kutoa mkopo sababu hizo ni mali za familia, kutoa mkopo bila ya ridhaa ya mmoja wa wanandoa ambapo ni batili," anasisitiza Teresia.

**SHINYANGA INATISHA**

Shinyanga ni miongoni mwa mikoa ambayo wanawake wamejiingiza kwenye mikopo hiyo, wakidaiwa kuwa wapo wengine wanaokopa bila kuwaarifu waume zao ambao hustuka pale ufilisi wa mali unapofika nyumbani baada ya mama kukwama kurejesha.

Itakumbukwa kuwa mkazi wa Tambukareli Manispaa ya Shinyanga Sarah Bundala (55) alidaiwa kujinyonga, baada ya kushindwa marejesho akihofia kuwa atapigwa na mumewe, sababu alishamkataza kujiingiza kwenye mikopo, lakini akakopa kwa kificho.

Mwezi uliopita mkazi wa Kambarage, Kulwa Juma, alitishia kuvunja ndoa baada ya mkewe kukopa bila ya kumtaarifu huku akashindwa kurejesha marejesho.

Analalama mama watoto wake hana kazi wala biashara kwanini amekwenda kujiingiza kwenye mikopo bila kumtaarifu?

"Siku moja nilitoka kazini nimepumzika ghafla nikashangaa watu wanabisha hodi wakaingia ndani na kujitambulisha ni wakopeshaji wamekuja kuchukua fedha zao au mali ambazo ziliwekwa dhamana, kwa kuwa sikuwa na taarifa wala fedha wakachukua vitu ndani na kutufilisi," anasema Kulwa.

Alitafakari na kuona si vyema achukue maamuzi ya haraka bali kutafuta ufumbuzi ndipo mkewe akamuomba msamaha, lakini ndani wamebaki kweupe kila kitu kimekwenda kwa wakopeshaji.

**KUKOSA UFAHAMU**

Zai Abdul mkazi wa Ndembezi, anasema chanzo ni baadhi ya wanawake kukopa wakati hawana biashara mbali na kufuata mkumbo wa marafiki na wanapopata fedha huzitumia kwenye starehe na wakati wa marejesho huanza kuhangaika.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Dome Kata ya Ndembezi, Solomon Najulwa, anasema hizo za mikopo zimekuwa zikisaidia akina mama wengi ambao wanania ya kufanya biashara, na wao ndiyo wamekuwa wakiwasainia barua za kuwadhamini ili waipate.

Anasema changamoto inakuja pale baadhi ya wanawake wanapokosa uaminifu na kudanganya kuwa wanabiashara kumbe hazipo na mikopo ambayo huichukua huenda kufanya mambo yao mengine na kushindwa marejesho, lakini wengine huenda kwenye shirika jingine kukopa ili fedha walipe mkopo wa awali.

"Unakuta mwanamke ana mikopo zaidi ya mitano na biashara hana, na dhamana ambayo ameweka kwenye mikopo ni vitu vile vile vile,

**INAENDELEA UK.12**

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Mgomo Kariakoo ulivyoibua ari ya kukutana na Waziri Mkuu

## •Wamo wa Handeni wadai TANROADS kuna jambo lao

WIKI inayomalizika inaandika historia kwa wafanyabiashara kutapika na kupandisha mukari wakieleza kwa kina na kinagaubaga kile kinachowachefua kwenye biashara sokoni Kariakoo Dar es Salaam.

Kilichosikika Kariakoo ni sehemu ndogo ya vilio na malalamiko mengi ya jumuiya mbalimbali za Watanzania ambao wana kero nyingi wanazotamani kuzitoa. Mfano kuna wasafirishaji kuanzia daladala hadi malori ya shehena, hawa wanapoanza siku kila hatua wanayotembea ni mkono, unaotaka kitu kidogo.

Wapo wawekezaji binafsi kwenye huduma za afya maabara, zahanati na hospitali na pia wapo waliojitumbukiza kwenye elimu wakijenga shule za msingi, sekondari vyuo na vyuo vikuu wana vilio vyao ni kilio cha vikwazo, kodi, tozo na ada.



Wakazi wa Kambulwa wakikusanyika kwenye maeneo yao kabla ya mkutano wa kujadili hatima yao. **PICHA: MWANDISHI WETU**

### VIJIJINI WAPO

Baadhi ya watu wanaotamani kukutana na Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa ni wakazi wa Kitongoji cha Kambulwa wakulima na wafugaji takribani 400, ambao wanaishi Kwamgome wilayani Handeni mkoani Tanga.

Wanacholia ni njaa, hawajalima masika wala vuli tangu mwaka jana baada ya ardhi yao kutwaliwa na serikali ili kuchimba kifusi, kokoto na mchanga kwa ajili ya ujenzi wa barabar a kutoka Handeni hadi Dodoma, ikipitia Manyara, Singida hadi Dodoma.

Wanapofika kwenye ofisi za Nipashe wanasema: " Sisi wananchi wa Kwamgome ni wafugaji na wakulima tunaolima eneo la Kambulwa, lakini maeneo yetu yamechukuliwa na Halmashauri ya Mji – Handeni kwa ajili ya kambi ya ujenzi, machimbo ya mawe, kifusi na kokoto za ujenzi wa barabara za kitaifa." Wanasema katika waraka wanaouwasilisha.

Waraka wao kwa Waziri Mkuu una malalamiko ya watu 22 wenye sahihi zao wakieleza kuwa Oktoba 16, 2022 walimwandikia Mkurugenzi wa Mji Handeni pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mkuu wa Mkoa Tanga na mbunge wa Handeni Mjini kuhusu malipo ya maeneo yao.

Wanasema ni sehemu wanayoitegemea kwa kilimo, makazi na ufugaji, wakihoji wanalipwaje kwa kuwa hawana sehemu ya kuishi, kufuga na kulima kwa ajili ya kupata chakula na kwamba muda wa kilimo tayari umepita wa vuli na masika na tayari ni miaka miwili sasa.

Wanasema katika barua yao kwa Waziri Mkuu Majaliwa, aliyoambatanisha na majina 22 ya wakalalamikaji, ambayo Nipashe ina nakala yake.

Wanaongeza kuwa maeneo yao yalishapimwa kisheria na kufanyiwa tathmini ya ardhi na hati wanazo kama sheria hiyo inavyotaka na kwamba tathmini ilifanyika Juni 16, 2022 na sasa ni karibu mwaka umepita.

Wanasema kuanzia Novemba 2022 uongozi wa mkoa umewapa maelekezo ya kufutafuta maeneo mengine wanunue na kwamba watalipwa. Hofu yao ni kwamba muda umeshapita, lakini leo hakuna majibu wala mawasiliano yoyote na serikali wakilalamika kuwa hawana sehemu za kuishi au makazi , malisho ya mifugo na kilimo na kuhoji wataishije?

Wanachotaka kwa Waziri Mkuu na serikali ni kujua msimamo wa serikali kuhusu malipo yao, wakihoji watalipwa lini? Wanashangaa kuona kampuni iko 'saiti' inachimba mawe, kifusi, kokoto na mchanga lakini hawajalipwa fidia inakuwaje?

Wanawageukia Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Mji Handeni mbona wako kimya bila kuwaeleza kuna tatizo gani? Watendaji wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Taifa na Mkoa kwa vile mradi huo umechukua makazi yao wangeongea nao lakini wote wamekaa kimya.

Katika barua ya malalamiko wakulima hao na wafugaji 22 wanasema kilichotokea kwa wafanyabiashara wa Kariakoo kitoe funzo viongozi wa serikali wahudumie na kujali wananchi hasa maskini ambao wanaoitegemea na kuiamini serikali kwa kila jambo.

### UTETEZI WA VIONGOZI

Zafarani Madayi ni Meneja wa Mazingira na Jamii TANROADS Taifa, anapoulizwa kuhusu madai ya wakazi wa Kwamgome, kuwa kampuni ya ujenzi (jina tunalo) imeshaingia kazini bila kuwalipa wananchi ambao ardhi imechukuliwa, anasema sheria zikifuatwa hakutakuwa na kulalamika.

Utaratibu na sheria unaelekeza kuwa kabla ya mkandarasi kuingia kwenye eneo kuchukua kifusi au kuanza kazi ni lazima awasiliane na uongozi wa eneo na awatambue wamiliki , waonyeshe mipaka yao, uthamini ufanyike, walipwe kisheria na wakubali kutoa maeneo yao yachimbwe mawe, mchanga, kokoto na kabla ya kufanya hayo sheria hairuhusu.

Zafarani anasema wanacholipiwa ni fidia ya ardhi na mazao na kwamba kama hawajapata haki yao waende TANROADS Mkoa wa Tanga, maana ina taarifa zote za barabara miradi mkubwa kwa midogo. Anawashauri kumchagua mwakilishi siyo waende kundi la watu 400 na baadhi ya vitu wanavyotakiwa kwenda navyo ni barua ya Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa au Kijiji au viongozi wa kata kuwathibitisha.

"Hata hivyo, wafuatilie na kujiridhisha kwanza kufahamu iwapo ardhi ni mali yao au ya kijiji maana kama ni ya kijiji hawatafidiwa badala yake halmashauri inayohusika italipwa mrahaba." Anasema Zafarani.

### TANGA YAWASHANGAA

Ofisi ya Meneja wa TANROADS Tanga, inakiri kuwa ardhi ya kitongoji cha Kambulwa imechukuliwa kwa ajili ya kupata kokoto, mchanga, mawe na kifusi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kilometa takribani 430 kuanzia Handeni kipita mikoa ya Manyara-Singida na Dodoma.

Hata hivyo, inawashangaa mbona hawajafikisha malalamiko yao ofisini humo? Inawakaribisha kwa Meneja wa Mkoa, wasilalamike wafike TANROADS na watapata majibu ya maswali yao na kwamba tangu kutangazwa hatua za kuchukuliwa eneo hilo hawajawasilisha malalamiko ofisi ya mkoa huo, anasema Meneja wa Mkoa, Eliazary Rweikiza.

Anawatoa hofu kuwa wamehamishwa eneo hilo, ili kuwalinda wasije kuumizwa na milipuko ya mawe na kwamba ni jambo linalofahamika hivyo wafike ofisi ya mkoa na watapatiwa majibu ya maswali yao anasema Rweikiza.

# MWANANDOA HILI NI SOMO MIKOPO UMIZA, KOMAA USIFILISIWE, SIMAMA NA SHERIA

INATOKA UK.11

akibanwa marejesho anakwenda kukopa kwingine ili apunguze deni hivyo anajikuta ana madeni lukuki," anawaonya Najulwa.

"Baada ya kukwama kulipa madeni wakopeshaji wanakwenda kumfilisi cha kushanghaza hata mume hajui ndipo mgogoro wa familia unapotokea, na tumekuwa tukipokea kesi nyingi mno za familia kufarakana na hata kuvunjika sababu ya mikopo,"anaongeza Najulwa.

UDANGANYIFU

Mkurugenzi wa taasisi ya ukopeshaji ya Msilikale, Robert Prosper, anataja taratibu za ukopeshaji mikopo, kwamba wanawake wanafika na wadhamini wao pamoja na barua kutoka kwenye uongozi wa serikali za mitaa huku wengine wakisema hawajaolewa, na hakuna ambaye analazimishwa kukopa bali hupewa mikataba na kuisoma na kuisaini.

Anasema baadhi ya wanawake si waaminifu, hudanganya kwa lengo la kupata mkopo, na wengine hawana biashara za kufanya na huazima biashara za marafiki zao kwa muda ili maofisa wetu wajiridhishe, kumbe walikuwa wakidanganya.

"Shida ambayo naiona ni wanawake kuikosa elimu ya ujasiriamali na wanakopa fedha hizi kwa mkumbo na sisi hutufilisi tu moja kwa moja, bali tunawasiliana kwanza na mteja wetu pamoja na kupitia kwa viongozi ambao walimpatia barua ya utambulisho, akikwama ndipo tunakwenda kuchukua vitu alivyoweka dhamana," anasema Prosper.

"Nawaomba wanawake sababu ndiyo wateja wetu wakubwa, waache kukimbilia mikopo kama hawana biashara na wengi ukiwafuatilia fedha hizi wakishachukua wanazitumia kwa mambo mengine tofauti na walivyoomba, fedha hizi zinahitaji uzizungushe kuendesha biashara yako ndipo upate marejesho," anaongeza.

Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Shinyanga Donasian Kessy, anasema kuna wakati walinusuru wateja ambao walikuwa hatarini kuuziwa nyumba kwa sababu ya mikopo umiza, lakini baada ya kufuatilia wakaona waachane na kuwasaidia kwani walifanya hivyo kwa hiara.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga John Tesha, anawashangaa wanawake kukimbilia kwenye mikopo na kufilisiwa wakati kuna fursa za mikopo asilimia 10 zinazotolewa na halmashauri.

Anasema tatizo la wanawake wamezoea kupewa fedha mkononi ambazo hukopeshwa ili wakageuze matumizi ikiwamo kupeleka marejesho kwenye maeneo mengine ambayo wamekopa, lakini halmashauri siku hizi hawatoi fedha bali wanaviwesha vikundi kununua vitendea kazi ndiyo maana wanakwepa kukopa.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Shinyanga, Lidya Kwesigabo, anasema migogoro ya familia ni moja ya sababu ambayo imekuwa ikisababisha ongezeko la watoto wa mitaani na wengine kuishi katika mazingira hatarishi sababu ya ukosefu wa malezi.

Anataja takwimu za watoto wa mitaani mkoani humo kuwa wapo 612 na watoto ambao wanaishi katika mazingira hatarishi ni 99,939.

ELIMU

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

# Masharti na kukosa mbinu utafutaji kunavyowakwamisha wenye ulemavu

ELIMU ya mbinu za utafutaji miongoni mwa wajasiriamali wanaoishi na ulemavu ni tatizo. Aidha, mwamko wa kutumia fursa ya mikopo inayotolewa na serikali ni mdogo, ikilinganishwa na wasio na ulemavu kutokana na vikwazo mbalimbali kama masharti ya mikopo hiyo.

Kutokana na vikwazo, idadi ya waliopata mkopo ni ndogo na kati ya vikundi 90 vya wajasiriamali wenye ulemavu vilivyosajiliwa Zanzibar ni 12 pekee vilivyopata fedha za mkopo wa UVIKO-19.

Ikumbukwe wakati wa janga la corona, serikali ilipata mkopo wa Shilingi bilioni 230 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kukabiliana na athari za maradhi hayo.

Wizara ya Masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar, ilitengewa Shilingi bilioni 31 kwa ajili ya wajasiriamli visiwani Zanzibar.

Fatma Mgwali Khamis, katibu wa kikundi cha watu wenye ulemavu mkoa wa Kaskazini Unguja cha Safinia yako, ambaye haoni anasema upatikanaji wa mikopo hiyo umekuwa na changamoto kubwa hasa kwa wenye ulemavu.

Anasema kikundi chao chenye wanachama 20 ambao wanajishughulisha na kazi za mikono za ufumaji ni mwaka pili sasa tangu kuomba mkopo huo hawajapata kitu.

"Tumeshakamilisha taratibu zote za kuomba mkopo huu mwaka wa pili hatujaingiziwa fedha na shughuli zetu za uzalishaji zimesita. Tumejaribu kufuatilia benki lakini wanasema hawajaona fomu ya maombi yetu,"anasema.

Anasema miradi yao imesimama kutokana na kukosa fedha za kununua malighafi inayotumiwa kufuma.

Fatma anataja malighafi wanazotumia kuwa ni kamba za usumba (makkumbi ya nazi) kwa ajili ya kufuma mazulia na mikoba ambayo soko lao kuu ni watalii.

Walipoomba mkopo walitarajia fedha hizo kuwaongezea mtaji ili kuzalisha bidhaa nyingi na kuwa na soko la uhakika.

"Hivi sasa tunapata tenda ya kuuza bidhaa zetu lakini hatuna kitu kwa sababu ya kukosa zana na nyenzo za kufanyia kazi kama tungepata mkopo tungeendeleza uzalishaji," anasema Fatma.

Fatma ambaye ni diwani viti maalum mkoa wa Kaskazini Unguja anaiomba serikali fedha hizo kupelekwa katika mabaraza ya miji ili kusaidia katika utaratibu uliowekwa.

Fatma anaungwa mkono na Njuma Ali kutoka kikundi cha watu wenye ulemavu wa kukindi hicho kinachojishughulisha na ufinyanzi.




Watu wanaoishi na ulemavu wanahitaji ujuzi na mikopo nafuu ili kujikomboa kiuchumi. **PICHA: MTANDAO**

Njuma, anasema siku zinayoyoma, fedha za mkopo hawajapata licha ya kukamilisha taratibu zote zinazohitajika ikiwamo kuwa na akaunti namba ya

kikundi na kujaza fomu ya mkopo, ambayo wameyakamilisha na muda umepita tena takribani mwaka sasa hakuna fedha walizopata.

Anasema waliomba mkopo baada ya Rais Dk. Hussein Mwinyi kusisitiza kuitumia fursa ya fedha za UVIKO-19 kujikwamua kiuchumi baada ya kuathiriwa na janga la maradhi hayo.

Mjasiriamali Nasra Hamad, mwenye ulemavu wa viungo ni mama lishe, anasema kuna usumbufu mkubwa wa kuomba mkopo huo na alikata tamaa mapema kuomba mkopo kutokana na vikwazo.Anashauri serikali kukutana na wenye ulemavu na kuwapa elimu jinsi ya kuomba mkopo huo ili kuondokana na usumbufu wanaokumbana nao.

"Kila siku tumekua tukirejeshwa kuwa maombi yetu hayajakamilika mara nenda huku mara kule hali ambayo imenikatisha tama," anasema.

Anasema watu wenye ulemavu wanahitaji mikopo nafuu kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini lakini pia kuondosha wimbi la ombaomba mitaani ambako wenye ulemavu wanaongoza kwa idadi.

**WAJUTIA MIKOPO**

Katibu wa kikundi cha Yajayo Yanafurahisha huko Kizimkazi Mkoa wa Kusini Unguja, Muhammed Abdallah, anasema nia ya mkopo huo ni nzuri lakini haujawanufaisha wenye ulemavu.

Anasema waliomba mkopo wa milioni 15 na kupatiwa 8,000,000 Machi mwaka jana, akikiri uwepo wa changamoto katika kuomba mkopo huo hadi kuupata akitaja harakati nyingi za kuanza usajili hadi kupata fedha.

"Kuna vipengele vingi kuanzia usajili nenda rudi ni nyingi lakini mkataba wao wa kurejesha malipo unatisha na sio rafiki kwa wenyeulemavu kama sisi," anaongeza Abdallah.

Anasema muda wa kurejesha ni kikwazo... "Tunaojishughulisha na kazi ya ushonaji tunatakiwa tukamilishe marejesho ya fedha tulizokopa ndani ya mwaka mmoja na nusu," anasema.

Muda ni mdogo hasa ikizingatiwa kuwa mauzo wanayouza si ya kiwango kikubwa na lazima wanatakiwa kurejesha fedha hizo za mkopo benki kila mwezi ni Shilingi 440,000, anaeleza Katibu.

"Fedha tuliyopatiwa yote tumenunulia vifaa vya kazi pamoja na mali ghafi....huu mkopo kwa kweli umetuweka roho juu maana hatuna faida tunayoipata, tunapouza bidhaa inatulazimu tuchangishane wanachama ili turejeshe benki kwa sababu mauzo yetu hayafiki 400,000 kwa mwezi."

Anasema hawataendelea tena kukopa baada ya kumaliza deni kwa sababu wanapitia wakati mgumu.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Watu Wenye ulemavu Zanzibar, Ussi Khamis Debe, anasema mikopo ya fedha za UVIKO-19 hasa kwa wenye ulemavu ni tatizo licha ya Rais Mwinyi kuagiza wapewe.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Watu Wenye ulemavu, Ussi Khamis Debe. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

"Sisi baraza tumechukua jitihada za kutengeneza vikundi vya watu wenyeulemavu maana vilikuwa vichache na hadi sasa viko 90 Unguja na Pemba, tulivyovisajili ili kutimiza masharti na tukaviunganisha na wakala wa uwezeshaji, kazi ipo katika utoaji wa mikopo kuna nenda, urudi nyingi mno,"anasema Debe.

Analeza kwa mshangao kuwa vikundi 90 vilivyoomba mkopo huo 12 ndivyo vilivyopata na baadhi ya vingine vinakataa kukopa kwa kuogopa kufilisiwa au kushtakiwa kwa kushindwa kulipa.

Anasema juhudi zinahitajika, kubadilisha mitazamo hasi ya vikundi hivyo ili kuitumia fursa ya kupata mikopo itakayowasaidia kujiendesha kiuchumi na kuachana na ombaomba.

Asha Aboud mwanaharakati wa kutetea haki za watu wenye ulemavu, anasema wanakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazokwamisha juhudi zao za kupata maendeleo.

Anazitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni ukosefu mitaji kwa sababu wengi hawakopesheki kutokana na uwezo mdogo.

Anasema zipo taasisi za fedha ambazo zinatoa fedha za mikopo kwa makundi mbalimbali kuendesha shughuli za ujasiriamali lakini kwa wenye ulemavu hayajafikiwa kikamilifu.

Mratibu wa jumuiya ya watu wasioona Zanzibar, Adil Muhammed, anasema wameitumia fursa hiyo ya mikopo lakini wengi wao hawakuzipata licha ya kufuata taratibu hivyo wamekata tamaa.

"Sekta nyingi zinapuuza kuwashirikisha wenye ulemavu hali inayosababisha kuwepo athari kubwa kwao lazima tushirikishwe katika utoaji wa ruzuku," anasema Muhammed ambaye haoni.

"Unapofatilia jambo lolote sisi tusiona huwa na changamoto kubwa sababu ina tulazimu tuongozane na atakayetuongoza kwa kila jambo ambaye inabidi umgharamie kila kitu. Unapofuatilia fursa kama hizi ukaambiwa njoo kesho, njoo kesho inatuvunja moyo na kutugharimu," anasema Muhammed.

Kassim Haji Mrisho Kaimu Mkurugenzi Idara ya Mitaji wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, anasema wajasiriamali na watu mbalimbali wamehamasika kuomba mikopo ya fedha za UVIKO-19 lakini kundi la wenye ulemavu ni wachache.

Anasema awamu ya kwanza imetoa mkopo wa Shilingi bilioni 15 kwa vikundi mbalimbali vya wajasiriamali ikiwamo ya watu wenye ulemavu.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Suleiman anasema serikali inasimamia kuona sheria ya watu wenye ulemavu inatekelezwa kikamilifu, lengo ni kuona haki za makundi hayo zinapatikana zikiwamo fursa za kiuchumi.

Harusi, anasema, sheria ya watu wenyeulemavu ya mwaka 2022 lengo lake ni kwenda na wakati na mabadiliko yaliopo sasa duniani ikiwamo mikataba ya kimataifa na kikanda kulinda haki za makundi hayo.

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA

# Zinaibuliwa mbinu kurejesha wasiopenda shule darasani



Wanafunzi wakitembea umbali mrefu, kupishana na vyombo vya usafiri kama magari na kuchafuliwa na vumbi. **PICHA: MTANDAO**

UNAPOONA watoto wanakataa shule, kuna jambo. Inawezekana wanaichukia kutokana na mazingira mabovu, umbali na njaa. Vyote ni sababu ya kukatisha masomo na kuichukia elimu.

Wapo ambao wanalazimika kuishia njiani na kufanya michezo na ikifika muda wa kurudi nyumbani wanarejea na wazazi au walezi wanaamini walikuwa masomoni.

Kwa wazazi na walezi wenye majukumu mengi au wagonjwa wasioweza kufuatilia na kukagua za wanafunzi wanaamini watoto wao walikuwa shuleni jambo ambalo ni tofauti hata baadaye akipewa taarifa kutoka shule na wanajamii wengine wanakuwa wagumu kuamini kwa kuwa kila siku watoto hao wanaaga wakielekea shuleni.

Shule kuwa mbali na makazi pia imekuwa ikiathiri wanafunzi wa kike ambao baadhi yao wamekuwa wakijiingiza kwenye zawadi za lifti za pikipiki na magari zinazozalisha mimba na kuwakatishia masomo.

Hali hiyo kwa sasa ni tofauti katika baadhi ya maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha ambayo imeanza kutatua kero hizo kwa kujenga shule maeneo yaliyokuwa na kero kama hizo.

Kibaha ni moja kati ya halmashauri tisa zinazounda mkoa wa Pwani ikiwa na kata 14, vijiji 26, vitongoji 102 na kaya 33,352 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka mwaka 2022.

Katika kata 14 ni sita pekee zilikuwa na shule za sekondari hivyo kufanya baadhi ya maeneo watoto kutembea umbali mrefu kufuata elimu kwa majirani.

Akizungumza na Nipashe Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Butamo Ndalahwa, anasema wapo wanafunzi ambao ufaulu wao ulikuwa unashuka kutokana na umbali wa shule na wakifika wanakuwa wamechoka huku wengine wakikatisha masomo.

Yote, yalirudisha nyuma kiwango cha ufaulu kwa halmashauri hiyo lakini pia kudumaza maendeleo kwa kuwa na vijana wachache wanaofikia na kuhitimu masomo.

"Kutokana na baadhi ya watoto kuwa na umri mdogo walishindwa kutembea umbali mrefu na kuchoka waliacha shule na kwenda kuchunga ng'ombe..." anaeleza.

Kwa mujibu wa Ndalahwa halmashauri ilipeleka fedha zilizotokana na mapato ya ndani kujenga vyumba vya madarasa, akitaja Sekondari ya Kawawa ambayo ipo pembezoni, iliyoanza kupokea wanafunzi.

Kadhalika, anataja juhudi za wananchi za kuanzisha ujenzi wa Sekondari ya Kawawa, ili kuwaondolea wanafunzi adha ya umbali mrefu kufuata shule ziliungwa mkono na serikali kuu iliyotoa fedha za kujenga vyumba vitano vya madarasa na matundu matano ya vyoo.

Mkurugenzi huyo anaendelea kueleza kuwa mbali ya umbali wa shule pia zipo ambazo zilikabiliwa na msongamano wa wanafunzi hali ambayo ilisababisha kushuka kwa ufaulu.

Anaeleza kuwa Shule ya Sekondari Disunyala ni kati ya mpya zilizoanzishwa kuondoa tatizo la msongamano kwenye shule nyingine na kwamba Shilingi milioni 112.5 zilitolewa kujenga vyumba vya madarasa vitano na matundu ya vyoo.

Awali shule hiyo ilipokea Shilingi milioni 100 fedha za UVIKO- 19, kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa matano na kuanza kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2023.

Shule hiyo ambayo iliyoanzishwa katika kata ya Kilangalanga ilikuwa na lengo la kupunguza msongamano tayari imepokea vyumba 10 vya madarasa na matundu ya vyoo ndani ya miaka miwili yanayohitajika na wanafunzi.

Katika hatua nyingine, Ofisa Elimu Sekondari, Fatuma Kisalazo anabainisha kuwa halmashauri hiyo ilipokea Shilingi milioni 940 kwa ajili ya ujenzi wa sekondari mpya mbili kupitia mradi wa kuinua Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

Anasema ujenzi huo umetekelezwa katika kata mbili za Gwata na Kikongo kwa kujenga vyumba nane vya madarasa, matundu 20 ya vyoo, maabara ya kemia, biolojia na fizikia, jengo la utawala, maktaba, tangi la maji la chini.

Fatuma anasema katika utekelezaji wa mradi huo kwa shule zote mbili, yapo majengo ambayo yamekamilika kwa asilimia 100, ikiwamo vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na mengine yapo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Halmashauri hiyo imetoa Shilingi milioni 172.9 zinazotokana na mapato ya ndani kwa ajili ya kuendeleza ujenzi na utengenezaji wa madawati na kwamba kila shule imepokea milioni 86.4.

"Sekondari hizi zimepokea wanafunzi 210 wa kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2023 na wanaendelea na masomo ujenzi wa shule hizi umepunguza vikwazo walivyokuwa wanakabiliana navyo vya kutembea umbali mrefu," anaeleza.

Aidha katika Kata ya Boko Mnemela ambayo haikuwa na sekondari na kusababisha wanafunzi wa maeneo hayo kutembea umbali mrefu hadi katika kata ya Soga wananchi walishirikiana na kuanzisha shule mpya ya Boko Mnemela kwa kuanza kujenga vyumba vya madarasa vitatu.

Fatuma anasema baada ya jitihada za wananchi serikali imetenga milioni 80 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vinne katika shule hiyo na Januari 2023 ilipokea wanafunzi 125.

Anasema shule shikizi zimeanzishwa kwenye kata ambazo wanafunzi wanatembea umbali mrefu ikiwamo Shule ya Msingi Masaki ambayo ipo kata ya Magindu, ambapo wanafunzi walikuwa wanalazimika kutembea zaidi ya kilometa 10 huku wengine wakikwama kutokana na umri kuwa mdogo.

Anasema serikali ilipeleka fedha zitokanazo na mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na sasa shule hiyo ambayo ipo pembezoni mwa halmashauri inapokea wanafunzi.

Anabainishwa kuwa shule nyingine shikizi zilizoanzishwa kwa ajili ya umbali ni Mkombozi iliyopo kata ya Kawawa ambayo ilijengwa kwa Shilingi milioni 100 fedha za UVIKO -19 zikijenga vyumba vitano vya madarasa na kwa miaka miwili tangu kuanzishwa wanafunzi 51 wameandikishwa.

Pamoja na ujenzi wa shule kwenye maeneo mbalimbali katika halmashauri hiyo pia suala la chakula shuleni limeendelea kuzingatiwa kwa utaratibu unaofanywa kati ya shule, walezi na wazazi lengo likiwa ni kuwapa chakula ili wasikwamishwe na njaa.

Mmoja wa wazazi wa Kata ya Kawawa Athumani Issa, anaeleza kuwa kuboreshwa kwa mazingira kutaleta hamasa kwa wanafunzi akisema wapo wanafunzi waliokuwa wakisuasua kutokana na kuchoka kutembea umbali mrefu huku wengine wakifeli kwa kukosa muda wa ziada wa kujisomea baada ya muda wa kawaida wa masomo.

Omari Hassan anayeishi Mlandizi anasema serikali kuimarisha miundombinu ya shule ni kuinua kiwango cha elimu na ufaulu kwani hakuna mzazi au mlezi atakayekubali mtoto asiende shule ambayo ipo karibu na mazingira ya nyumbani na pia ni bora.





## Mradi mifumo afya waboresha utoaji huduma

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MRADI wa kuboresha mifumo ya afya (Project ECHO), umetajwa kuleta manufaa makubwa katika kuboresha utoaji huduma za afya nchini.

Akizungumza jana kwenye kikao cha kamati tendaji ya mradi huo iliopo chini ya Wizara ya Afya, Msajili wa Baraza la Wataalamu wa Maabara, Mary Mtui, kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Serikali, alisema mradi huo umeongeza idadi ya wataalamu wa afya wanaoshiriki katika mafunzo kwa njia ya mtandao, yanayotolewa katika vituo tisa (hubs) vilivyofunguliwa nchini.

Alisema mradi huo unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) na mafunzo hayo yanatolewa na wataalamu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe.

"Inatia moyo kuona idadi ya washiriki wa mafunzo inaongezeka kila siku na hii inatokana na jitihada kubwa zilizofanywa na wataalamu wa Chuo Kikuu Mzumbe kupitia mradi wa kuboresha mifumo ya afya nchini unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia CDC. Kikubwa Mzumbe waongeze kasi ya kutoa CPD Points (alama za ufaulu) kwa washiriki," alisema.

Alisema alama wanazopata washiriki kwenye mafunzo zinazowaongezea washiriki nafasi ya kuhuisha leseni zao na baadhi kupanda madaraja.

"Chuo Kikuu Mzumbe waongeze kasi ya kutoa CPD points kwa wakati ili kuongeza idadi wa washiriki wa mafunzo ambayo yamekuwa yana manufaa makubwa katika kuboresha utoaji huduma za afya nchini," alisema.

Alisema katika kikao hicho wanakusudia kujadili na kuweka mikakati ya namna ya kuongeza ushiriki wa wataalamu wa afya katika mafunzo kwa njia ya mtandao (ECHO Platforms) pamoja kutolewa alama hizo kwa wakati.

"Kwa sasa mafunzo hayo yanaendeshwa kila wiki kupitia vituo tisa na washiriki kufuatilia mafunzo hayo kupitia kliniki zaidi ya 399 zilizofungiwa vifaa vya mafunzo nchi nzima," alisema.

Mtui alisema zaidi ya watumishi na watoa huduma za afya 650 wanashiriki mafunzo nchini nzima kila wiki na kwa sasa Mzumbe kwa kushirikiana na Baraza la Madaktari Tanzania (MCT), wanaendelea kuchakata maombi mapya ya zaidi ya 2,600 kwa washiriki waliokidhi vigezo vya ushiriki kwenye mafunzo.

Wakichangia mkutano huo, wadau walipongeza serikali na wadau wa maendeleo CDC kwa kuwekeza katika mfumo wa mafunzo kwa njia ya mtandao ili kuwajengea uwezo wataalamu wa afya wakiwa mahali pa kazi.

Awali, Mratibu wa Project ECHO Tanzania, Jacob Lusekelo, alisema wizara inakusudia kuendelea kushirikiana kwa karibu na wadau mbalimbali wa maendeleo nchini ili kupanua wigo wa mafunzo na usimamizi nchini.

# Mwongozo uendeshaji kilimo korosho watolewa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MWONGOZO wa uendeshaji wa mashamba ya korosho wilayani Manyoni, mkoani Singida umezinduliwa ili kuongeza usimamizi na ubora wa zao hilo na tija iliyokusudiwa.

Mkuu wa wilaya hiyo, Kemilembe Lwota, alizindua mwongozo huo jana alipokutana na wadau wa zao la korosho wa Mkoa wa Singida kwa lengo la kuupitisha na kuuzindua kwa ajili ya uendeshaji wa mashamba makubwa ya pamoja.

Alisema mwongozo huo utasaidia kutatua tatizo la usafishaji wa mashamba na utoaji wa huduma za ugani na kila mkulima atalazimika kufuata utaratibu uliopo kwenye mwongozo.

"Tutaupitia mwongozo wetu wa mashamba ya korosho ambao utasaidia kuhudumia na kusimamia mashamba hayo hasa kusafisha na huduma za ugani," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho, Francis Alfred, aliushukuru uongozi wa wilaya kwa kusimamia kikamilifu uwekezaji wa mashamba ya korosho.

Alisema bodi imejenga ofisi na kuweka watumishi wilayani Manyoni na kuwapatia vitendea kazi kama pikipiki ambazo zitawasaidia kuyafikia mengi na kutoa huduma za ugani kwa weledi zaidi.

Aliwataka wakulima wanaoishi nje ya Wilaya ya Manyoni kuweka vibao vinavyotambulisha majina ya wamiliki pamoja na namba za simu ili wawasiliane nao kwa ajili ya kuwapa ushauri.

"Tumejenga ofisi katika mashamba ya pamoja na kuweka watumishi ambao tumewapatia pikipiki ili waweze kutoa huduma kwa wakulima wa Manyoni, Itigi na Ikungi, hata hivyo tunawaomba wakulima wa nje ya hapa kuweka vibao na namba zao za simu ili wataalamu wetu waweze kuwashauri," alisema.

Alisema, wamejipanga kufanya mnada wa korosho kwa wakulima na wana kilo 23,000 sawa na tani 23.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manyoni, Heri Kaombwe, alisema bado serikali imeendelea kusafisha mashamba hayo na kuyasajili Wizara ya Ardhi na kila mkulima atahitajika kwenda kuchukua ankara zao katika ofisi hizo.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (katikati), akikata utepe kuzindua kitabu cha Kanuni Bora za Kilimo cha Chai na cha Mwongozo wa Mkulima wa Chai, katika sherehe ya Siku ya Chai Duniani, yenye kaulimbiu uzalishaji na masoko endelevu ya chai kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi Tanzania, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Chai haitaruhusiwa kuuzwa nje bila kupita mnadani'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema mnada wa zao la chai unatarajiwa kuanza mwezi Juni mwaka huu na mfanyabiashara yeyote hataruhusiwa kuuza chai nje kama haijapita kwenye mnada.

Aidha, ameagiza kutozwa faini kampuni ambazo hazijawalipa wakulima.

Aliyasema hayo juzi wakati wa hafla ya uzinduzi wa kitabu cha mwongozo cha mkulima wa chai ulioambatana na Siku ya Chai Duniani iliyofanyika jijini hapa.

Alisema mnada huo utafanyika jijini Dar es Salaam na kutakuwa na bei yenye tija kwa wakulima wa zao hilo.

Pia aliagiza Bodi ya Chai nchini iache kufanya kazi kupitia takwimu za zao hilo zilizopo kwenye kablasha, badala yake wabuni mkakati wa kutoka kwenye uzalishaji mdogo na kufikia uzalishaji mkubwa kwa mwaka.

"Wakulima wanatakiwa kufanya kilimo ambacho kitawainua kiuchumi hivyo nyie bodi hakikisheni mikakati yenu inainua kilimo cha chai," alisema Bashe.

Kuhusu madeni ya wakulima wadogo, Waziri Bashe aliagiza Mkurugenzi wa Bodi hiyo kuzitoza faini kampuni hizo ili wakulima walipwe waendelee na maandalizi ya msimu mwingine.

"Inakuwaje kampuni haziwalipi wakulima halafu mziangalie hakikisheni wanatozwa faini," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Chai Tanzania, Mary Kipeja, alisema moja ya kero kubwa waliokuwa nayo ni pamoja na kuwa uzalishaji mdogo ilhali wana maeneo makubwa ya kulima na upotevu wa majani mengi shambani.

Pia soko la zao hilo nchini lipo chini na wakulima wanafanya kilimo ambacho hakina tija.





# Tatizo sumu kuvu kwenye mazao lapatiwa ufumbuzi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

TATIZO la sumu kuvu na upotevu wa mazao ya nafaka baada ya mavuno ambalo limekuwa likiwakabili wakulima kwa muda mrefu wilayani Mbarali, Mkoa wa Mbeya, limepatiwa ufumbuzi baada ya kugundulika kwa mashine maalum yenye uwezo wa kukausha mazao kwa muda mfupi hata wakati wa msimu wa mvua.

Mashine hiyo imegunduliwa na kampuni inayojihusisha na uuzaji na usambazaji wa zana ya Agricom Africa Ltd na kuzinduliwa wilayani Mbarali kwa ajili ya kuokoa mazao ya wakulima.

Wakizungumza wakati wa hafla ya kuzindua mashine hiyo, baadhi ya wakulima wa mpunga wilayani Mbarali walisema kuwa kabla ya ugunduzi wa mashine hiyo, mazao yao yalikuwa yakiharibika hasa wakati wa msimu wa mvua na walishindwa kuyakausha.

Mmoja wa wakulima hao, Getruda Barnabas, alisema kila mwaka zaidi ya asilimia 10 ya mazao yake aliyokuwa akivuna wakati mvua ikinyesha yalikuwa yakiharibika kwa kushindwa kukauka.

"Kila mwaka mazao yangu yalikuwa yakiharibika hasa wakati wa msimu wa mvua ambapo jua haliwaki kwa muda mrefu, nilikuwa napoteza mazao mengi kwa kuyatupa baada ya kuoza huku mengine yakivunda na kuota kuvu kutokana na kuhifadhiwa ndani kwa muda mrefu wakati nikisubiri jua liwake ili niyaanike," alisema Getruda.

Asajile Mwalukasa, alisema kugunduliwa kwa mashine hiyo kutasaidia kuongeza ubora wa mazao yao na watakuwa na uhakika wa kuyauza kwa bei nzuri.

"Huwa tunavuna mazao bora sana kutoka shambani, lakini yanapokosa jua la kuyakausha vizuri yanaonekana kuwa dhaifu na kutulazimu kuyauza kwa bei ndogo, lakini sasa tunaamini kuwa kuwapo kwa mashine hii kutatuondolea changamoto hiyo," alisema Mwalukasa.

Meneja wa Kampuni ya Agricom Afrika Ltd Kanda ya Nyanda za Juu kusini, Joseph Manoni, alisema kuwa mashine hiyo itawasaidia wakulima kuvuna mazao bora na kuyafikisha sokoni yakiwa katika hali nzuri.

"Tunawaletea wakulima mashine hii ili iwasaidie kuboresha shughuli zao ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kuvuna mazao bora na kuyafikisha sokoni yakiwa katika hali nzuri yenye ubora unaokubalika," alisema Manoni.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Mbarali, Joshua Halinga, aliwataka wakulima kuikubali teknolojia hiyo na kuitumia kwa lengo la kujinufaisha kiuchumi.

Akizindua mashine hiyo, Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Oliver Sulle, aliwataka wakulima wa mpunga wilayani humo kuchangamkia fursa hiyo ili kukabiliana na hasara waliyokuwa wakiipata.



Wakazi wa Mtaa wa Sai- Ituha, Kata ya Ilomba jijini Mbeya jana wakionyesha mazao yao yaliyofyekwa na watu wanaodaiwa kuchukua kandarasi ya kujenga ukuta wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania Tari kituo cha Uyole ili kuzuia wakazi hao kulima mazao katika eneo hilo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# LATRA kuanza ukaguzi magari yanayosafirisha bidhaa hatarishi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa ardhini (LATRA), imesema itaanza kutumia sheria ya ukaguzi wa magari yanayosafirisha bidhaa hatarishi kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda nchi jirani kupitia barabara zote nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Saluo, alisema hayo mwishoni mwa wiki mkoani Mbeya kwenye mkutano wa wadau uliolenga kupokea maoni kuhusu rasimu ya kanuni mpya za mamlaka hiyo, kilichoandaliwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Alisema kati ya kanuni nane zinazowasilishwa kwa wadau ni usafirishaji wa bidhaa hatarishi ambayo imelalamikiwa kwa miaka mingi na madereva kutokana na madhara wanayopata kiafya na wengine kupoteza maisha.

"Asilimia kubwa waathirika ni madereva na watu wanaopita jirani na magari yanayosafirisha kemikali hivyo endapo sheria ikapitishwa kuna uwezekano wa kuondokana na tatizo hilo," alisema Saluo.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, Andrew Magombana, alisema wizara inatambua vikwazo wanavyokabiliana navyo madereva kwenye sekta ya usafirishaji na wamekuja kufanya kikao na wadau kukusanya maoni.

"Tunaamini wadau mmepitia sheria na kanuni hizo nane zilitengenezwa zikiwapo za kusafirisha bidhaa hatarishi, tiketi mtandao, mfumo wa ufuatiliaji wa mienendo ya magari na nyinginezo," alisema Magombana.

Dereva Raimona Mwantoke, alisema kazi ya udereva ina vikwazo vingi ikiwamo usafirishaji holela wa kemikali zenye sumu na kuathiri pia wananchi wanaoishi kando ya barabara hizo kutokana na kuwapo kwa barabara kuu moja ya Tanzania na Zambia (Tanzam).

Msimamizi wa sekta ya usafirishaji Mkoa wa Mbeya, Amani Martin, alisema serikali imekurupuka kuleta mapitio ya sheria hizo kwa madai hawakushirikishwa kwenye hatua za awali.

# Operesheni watoto waendesha bajaji, bodaboda yaanza

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya, Kikosi cha Usalama Barabarani, kimeanza utekelezaji wa agizo la Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera, kufanya operesheni ya kukagua leseni za madereva bajaji na bodaboda ili kudhibiti wimbi la watoto kuendesha vyombo hivyo na kusababisha ajali.

Hivi karibuni Homera, alitaka ukaguzi wa leseni uanze mara moja kuanzia majira ya saa 12 jioni ili kuwakamata watoto waliojiingiza kwenye udereva bila kuwa na leseni hali inayohatarisha maisha ya watumiaji wengine wa barabara.

"Kwa uchunguzi wangu nimeona idadi kubwa ya watoto kuendesha bajaji na bodaboda, sasa hali hiyo ni kinyume na sheria za usalama barabarani, naomba Jeshi la Polisi muanze operesheni ya kukagua leseni ili kuangalia ukubwa wa tatizo hili ambalo linasababisha kero barabarani," alisema Homera.

Aliwataka madereva kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kukabiliana na wimbi la ajali ambalo kwa muda mrefu linasumbua Mkoa wa Mbeya.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama barabarani, mkoani hapo, Yusuph Kamotta, alisema miongoni mwa vyanzo vya ajali ni makosa ya kibinadamu ikiwamo mwendo kasi, uchovu, msongo wa mawazo.

Alisema vyanzo vingine ni ubovu wa magari na kuwasihi madereva kutokubali kuendesha vyombo vya moto vibovu hata kama wanalazimishwa na mabosi wao na kutoa taarifa za siri kwa polisi ili kuyakamata magari ya namna hiyo.

"Pia kuna tatizo cha wananchi kutozingatia sheria za usalama barabarani na badala yake kuvuka kwenye maeneo yasiyokuwa rasmi na kusababisha ajali, lakini pia madereva wengi kutokuwa na elimu ya matumizi ya alama za usalama barabarani," alisema Kamanda Kamotta.



## Wazanzibari wapewa fursa ununuzi nyumba mpya ZHC

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC), Mwanaisha Ali Said, amewataka Wazanzibari kuitumia fursa ya kununua nyumba mpya zinazojengwa na shirika hilo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari hizi, alisema nyumba hizo zinazojengwa eneo la Mombasa nje ya mji wa Zanzibar ni za gharama nafuu na zitasaidia kuondoa changamoto ya makaazi.

Alisema shirika hilo linajenga nyumba za makaazi na biashara katika eneo hilo ambazo zina ghorofa na zenye mandhari mazuri.

Akitaja bei ya nyumba hizo alisema, yenye vyumba viwili itauzwa kwa Sh. milioni 136 na yenye vyumba vitatu itauzwa kwa Sh. milioni 157.

Aidha, alisema utaratibu wa kuuza nyumba hizo utakuwa wa fedha taslimu na kwa njia ya mkopo kutoka taasisi za kifedha ikiwamo Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na Benki ya CRDB.

"Njia nyingine, ni malipo ya awamu ambapo mteja atatoa asilimia 30 ya nyumba anayoitaka na baada ya miezi mitatu atatakiwa kulipa asilimia 15 na baadaye atalipa asilimia 20, asilimia 25 na asilimia 10 ambapo mtu atatakiwa kulipa fedha hizo ndani ya miezi 13," alisema.

Pia shirika linatarajia kujenga nyumba za makaazi katika eneo la Nyamanzi, Saateni na maeneo mingine kwa ajili ya kukodishwa wananchi.

Alimpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa kulisaidia shirika hilo kufikia malengo yake ya kuwa tasisi inayoongoza katika sekta ya biashara ya nyumba Zanzibar.

Mradi wa nyumba za Mombasa umeanza Machi mwaka huu na unatarajiwa kumalizika Julai 2024, unagharimu Sh. bilioni 9.8 kati ya fedha hizo Shilingi bilioni tatu zinatoka Shirika la Nyumba na fedha zilizobaki zinatoka serikalini.

# ACT yahoji utoaji wa zabuni ubinafsishaji Bandari ya Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo Zanzibar, kimeitaka serikali ya Zanzibar kueleza zabuni ya ubinafsishaji wa Bandari ya Zanzibar ilitangazwa lini ili wananchi wapate kufahamu maslahi ya nchi yamezingatiwa vipi katika mkataba wa ubinafsishaji.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Habari na Uenezi wa chama hicho, Salum Bimani, wakati akihutubia mkutano wa hadhara uliofanyika katika viwanja vya Alabama Mjini Unguja na kuhudhuriwa na Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud.

Bimani alisema bandari ni idara nyeti kiuchumi na haikuwa muafaka kubinafsishwa badala ya kuendeshwa na serikali kutokana na umuhimu wake hasa kwa kuzingatia Zanzibar ni nchi ya visiwa.

"Tunataka serikali itueleze zabuni ya ubinafsishwaji wa Bandari ya Malindi umefanyika lini na zabuni yake imetangazwa lini ili wananchi wapate kufahamu na sio mwafaka wa mambo kufanyika kinyemela," alisema.

Aidha, alisema ameshangazwa na hatua ya serikali kuvunja Uwanja wa Amani ambao una historia kubwa kwa Zanzibar baada ya Mapinduzi wakati ilikuwa na uwezo wa kujenga sehemu nyingine na uwanja huo kuendelea kubakia kuenzi historia ya Zanzibar.

"Tunataka kufahamu ni nani ameidhinisha uwanja wa Amani kuvunjwa wakati una historia kubwa kwa Zanzibar kama serikali imeamua kujenga uwanja wa kimataifa kwa nini wasijenge sehemu nyingine badala ya kuvunja historia ya Zanzibar kwa uwanja wa Amani," alisema Bimani.

Naye Mwenyekiti wa chama hicho, Juma Duni Haji, alisema Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ana deni hajalitekeleza kuhusu mambo ya msingi waliyokubaliana ya maridhiano na marehemu Seif Sharif Hamad kabla ya kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa mwaka 2020 baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu.

"Kuna mambo ya msingi ya makubaliano walioyafikia kati ya Dk. Mwinyi na marehemu Maalim Seif mpaka sasa hayajatekelezwa na tumechukua hatua za kumkumbusha ili kuweka mazingira mazuri kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025," alisema Juma Duni.

Alisema uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ulitawaliwa na uvunjaji wa haki za binadamu na zaidi ya watu 21 walipoteza maisha kwa kupigwa risasi na wengine kupata ulemavu wa maisha jambo ambalo halipaswi kujirejea katika uchaguzi ujao wa 2025.

"Tumeandika kitabu cha uvunjaji wa haki za binadamu uliojitokeza mwaka 2020 na kitabu hicho nimeshawakabidhi akiwamo Rais wa Zanzibar, Waziri Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili mambo haya yasiendelee kujitokeza katika ujenzi wa demokrasia na utawala bora Zanzibar," alisema.

Aidha, alisema inasikitisha kuona vitendo vya ubaguzi vinajitokeza Zanzibar wakati ni kinyume na misingi ya mapinduzi ambayo yaliondoa ubaguzi wa rangi, ukabila, jinsia na kuleta usawa kwa wananchi wote wa Zanzibar. Alisema hivi sasa Zanzibar kuna watu wanabaguliwa katika ajira kutokana na eneo wanalotoka na itikadi ya kisiasa jambo ambalo linakwenda kinyume na misingi ya Mapinduzi ya mwaka 1964 na malengo ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Akizungumzia Katiba mpya ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Duni alisema Rais Samia anastahili kupongezwa kwa kurejesha mchakato wa Katiba mpya baada ya kukwama katika hatua ya kupigiwa kura ya maoni.

Alisema mambo yaliojitokeza katika mchakato wa Katiba hadi wapinzani kuamua kususia, CCM Zanzibar ndiyo wanaopaswa kulaumiwa kupitia wajumbe wao wa Bunge la Katiba ambao walikwenda kinyume na msimamo wa pamoja waliotoka nao Zanzibar ikiwamo muungano wa serikali tatu.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais Othman Masoud Othman, alisema Zanzibar haiwezi kupiga hatua ya maendeleo kabla ya kuwa mamlaka kamili katika mfumo wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Alisema, mfumo wa Muungano unaotumika sasa, umekua kikwazo katika kuhakikisha maendeleo ya Zanzibar ndiyo maana chama cha ACT kinaendelea kuchukua juhudi za kuona Katiba mpya inapatikana ili mambo ya msingi ya Zanzibar kujiamulia yaweze kupatikana ikiwamo fursa za kiuchumi na uhusiano wa kimataifa.

Alisema kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022 asilimai 67 ya idadi ya watu ni vijana ambao wanahitaji kuona Zanzibar mpya yenye muono ya msingi ya maendeleo badala ya ndoto katika kuelekea mabadiliko ya maendeleo ya Zanzibar.

Mikutano ya hadhara ya Zanzibar imeanza kufanyika huku Chama cha ACT - Wazalendo kikiitisha mikutano zaidi ya vyama 22 baada ya kuzuiwa kwa muda mrefu.




Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar, Seif Mwinyi, akizungumza na wakulima na wadau wa kilimo visiwani humo hivi karibuni kwenye kikao cha wadau wa mbegu. Kushoto ni Mkurugenzi wa Umoja wa Wakulima wa Matunda na Mboga, Khamisi Mohamed, (kulia) ni Mwenyekiti wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania, Apolo Chamwela. **PICHA: ZUWENA SHAME**

# Benki ya Amana yazindua mikopo ya Hijja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA jitihada za kupanua wigo na huduma za kifedha, Benki ya Amana imezindua huduma mpya ya mkopo maalum wa safari ya ibada ya Hijja na Umrah ambao unalenga kuwawezesha waumini wa dini ya kiislamu kufanya ibada hiyo kwa gharama nafuu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma hizo mjini Unguja, Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaabi, amepongeza benki hiyo kwa kuanzisha huduma hiyo ambayo inawarahisishia waumini wa kiislamu kutekeleza ibada hiyo kwa haraka na gharama nafuu.

Alisema kumsaidia mtu katika jambo jema benki hiyo inastahiki kusifiwa kwa kuwawezesha watu kwa kumpatia mkopo ni bora zaidi ili kutekeleza jambo la kheri.

"Huu ni utaratibu mzuri muuendeleze na mtakuwa kigezo chema kwa taasisi zingine katika kuwawezesha wananchi masuala mbalimbali ya kheri," alisema Mufti.

Aidha, aliwataka Waislamu wenye uwezo kwenda hija wakiwa bado wana afya njema badala ya kusubiri mpaka wawe wazee na kukabiliwa na changamoto ya maradhi mbalimbali.

Mwenyekiti wa umoja wa taasisi za Hijja na Umra Zanzibar, Yusuf Salim Ali, alisema uwapo wa huduma hiyo ni suluhisho la changamoto ya muda mrefu ya uhaba wa fedha kwa waumini wa dini ya kiislamu ambao wana nia ya kwenda kufanya ibada hiyo.

Mkurugenzi wa huduma na kinga kutoka Benki ya Amana, Jamal Juma, alisema lengo la kuanzisha kwa huduma hizo ni kuwaondoshea vikwazo waumini wenye nia ya kutekeleza ibada hiyo.

Alisema imekuwa vigumu kwa watu wengi kumudu gharama za ibada hiyo kwa pamoja na huwalazimu kutumia muda mrefu kuweka hakiba mpaka kufikia kiwango cha gharama hizo.

Aidha, alisema katika kuendelea kujali umuhimu wa jambo hilo kuna watu hupata changamoto wanapoweka akiba yao ya fedha kwa ajili ya ibada hiyo, lakini inapofikia wakati gharama hupanda na benki hiyo itawawezesha kuwalipia asilimia 10 na kurejesha kiwango hicho baada ya kumaliza ibada hiyo bila ya riba yoyote.

Kwa mwaka huu Zanzibar inatarajiwa kusafirisha waumini zaidi ya 2,000 kutekeleza ibada hiyo huko Saud Arabia na waumini wa mataifa mbalimbali ulimwenguni hujumuka pamoja kutekeleza ibada hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**HAGAI ENOCK** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S0330/0140** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI TANZANIA MWAKA **1991** KUPITIA SHULE YA SEKONDARI MBEYA.YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.
TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/162184/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ABUU S NDUNGURU**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA SANLG YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 430 AEQ.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/385237/2022.**

**Fomu Na. 3**
**(Form No. 3)**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**(THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA)**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**(THE JUDICIARY)**
**MAHAKAMA KUU DIVISION YA KAZI**
**(LABOUR DIVISION OF THE HIGH CORT)**
**(Rule 16)**
**Samansi**
**(Summons)**
**(Made under labour Court Rules, Rule 16 GN. 106/2007 and O.V.R. 1 & 2 of CPC Cap 33 RE 2002)**
**LABOUR EXECUTION NO. 2 OF 2023**
**(Complain/Appeal/Application/Review/Revision/Referral (Reference) No.**
**MANSOOR ALLY RAJABU..........Mlalamikaji/mwombaji/Applicant**
**VS**
**SIMBA SUPPLY CHAIN SOLUTION LIMITED...............Mlalamikiwa/Mjibu Maombi/Respondend**

Unatakiwa kufika binafsi mbele ya Mahakama hii ikikaa SONGEA mnamo tarehe 29 Mwezi June Mwaka 2023 saa 10:00 Asubuhi Mbele ya Mhe E. ENYEMBELE, NAIBU MSAJILI na kubakia Mahakamani hadi uruhusiwe na Mahakama kuondoka, kwa ajili ya KUTAJWA/KUSIKILIZWA kwa maombi madogo na unatakiwa kujibu hati ya kiapo ndani ya siku kumi na tano (15).
(You are required to appear in person before this Court at........on the..........day of....20 at (time)....
Before Hon..............and to remain in attendance until permitted by the Court, for mention/hearing of revision/miscellaneous/dispute/execution and file counter affidavit within fifteen days (15).
Na unatahadharishwa kuwa usipuuze asilani kutii samansi hii vinginevyo utaadabishwa kwa kutozwa faini au kufungwa jela.
(You are further cautioned that you shall on no account neglect to comply with this summons lest you render yourself liable to a fine or imprisonment)
Imesainiwa hapa SONGEA siku ya jumanne tarehe 12 mwezi May, Mwaka 2023.

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
SONGEA

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOSEPH PAUL MABULA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1029-0092 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia NASSA SEKONDARI mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **SIM/BUS/RB/164260/2023.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**HABIBA K. NDOTO** anatangaza kupotelewa na cheti cha Kidato cha Nne chenye index namba **S3099/0007/2014** kilichotolewa na Shule ya Sekondari Doma chini ya Baraza la Mitihani la Taifa 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MOR/MOR/RB/169875/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NDUGU SAID ROBERT KONYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** rangi Nyeusi yenye namba za usajili MC 765DAU.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**KAT/MPA/RB/173453/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SALMIN SAIDI ALLY**
anatangaza kupotelewa na kadi ya **PIKIPIKI** yenye namba za usajili **T721AJR. YENYE CHASES NAMBA: MD221602358. ENGINE NO; MD17E16023.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/167525/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **DANIEL ELISAMIA NNKO** anatangaza kupotea na kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye usajili namba **T.809 AMH.**
Yenye Chassis Namba: **KZ900008955** na Engine Namba: **LJ780005835**
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa **Polisi:TAN/RB/172065/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MBINGA**
**MBINGA**
**SHAURI LA MADAI NO. 12/2023**
**AMSEK SECURITY SERVICE LIMITED......MDAI**
**DHIDI YA**
**COMPANY LIMITED (CHICO LTD).......MDAIWA**

**KWA: CHIKO LTD.**

Unaamuriwa kufika mahakamani tarehe **25/05/2023** saa mbili na nusu asubuhi siku ambayo shauri la madai mtajwa hapo juu limepangwa kusomwa hukumu.

Imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe **22/05/2023**

***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Russia yaitupia Dnipro makombora 16

**KYIV,** Ukraine

JESHI la Ukraine limesema vikosi vya Russia vimeulenga mji wa mashariki wa Dnipro usiku wa kuamkia jana kwa makombora 16 na mashambulizi 20 ya droni zilizotengenezwa nchini Iran.

Kamandi ya Jeshi la Ukraine aliyabainisha hayo kupitia ukurasa wake wa mtandao wa Facebook kuwa mashambulizi hayo dhidi ya wanajeshi na miundombinu yalifanyika kwa kutumia aina mbalimbali za makombora na droni chapa ya Shahed zinazotengenezwa nchini Iran.

Alisema mifumo yake ya ulinzi wa anga ilifanikiwa kuziharibu ndege zote 20 zisizotumia rubani pamoja na manne kati ya makombora 16.

Ilielezwa kuwa Dnipro ni mji mkubwa wenye wakazi takriban milioni moja kabla ya vita, ukiwa umbali wa karibu kilomita 125 kutoka safu ya sasa ya mapigano, huku maofisa wakisema kwamba ukubwa wa mashambulizi yaliyofanyika usiku wa kuamkia jana ulikuwa hauna kifani.

**Vita vya miinuko mikubwa kwenye ubavu kaskazini na kusini mwa vitongoji vinaendelea.**

Gavana wa Mkoa Sergiy Lyask aliandika kwenye mtandao wa Telegram kwamba vikosi vya Ukraine vilihimili mashambulizi ya wahasimu wao na kuongeza kuwa jumla ya watu wanane walijeruhiwa katika mashambulizi hayo, akiwamo mwanaume mwenye umri wa miaka 25 aliyejeruhiwa katika shambulizi la kombora katika wilaya moja na saba wakiwamo wanawake wawili katika wilaya nyingine.

Wakati hayo yakijiri, mkuu wa kundi la mamluki wa kijeshi wa Russia Wagner Yevgeny Prigozhin, alisema kuwa vikosi vyake vitaondoka Bakhmut mwishoni mwa mwezi huu na kukabidhi udhibiti wa mji huo kwa jeshi la Russia.

"Wagner itaondoka Artemovsk kutoka Mei 25 hadi Juni mosi," Yevgeny Prigozhin alisema katika rekodi ya sauti kwenye mtandao wa Telegram.

Inaelezwa kuwa Bakhmut awali ilijulikana kama Artemovsk, kwa heshima ya mwanamapinduzi wa Soviet, kabla ya Ukraine kuibadili jina.

Prigozhin alisema mamluki hao walikuwa wameweka safu za ulinzi kwenye viunga vya magharibi mwa mji huo kabla ya uhamisho uliopangwa wa udhibiti wa mji huo kwa jeshi la Russia.

Hata hivyo, Ukraine ilisisitiza kuwa vikosi vyake vilikuwa vinaendelea kusonga mbele pembezoni mwa mji huo ulioharibiwa, ingawa kasi yao ya kusonga mbele ilikuwa imepungua, huku Russia ikileta wanajeshi zaidi.

Pia Russia ilidai kwamba ilikuwa imeuchukuwa kikamilifu mji wa Bakhmut, lakini maofisa wa Ukraine wamesema tangu wakati huo kwamba vikosi vya Kyiv vinaendelea kudhibiti sehemu ndogo ya mji huo.

Naibu Waziri wa Ulinzi, Hanna Malyar, alieleza kuwa Ukraine ina udhibiti mdogo ndani ya mji huo na kwamba mapigano bado yanaendelea.

Malyar alisema wanajeshi wa Kyiv wameendelea kudhibiti wilaya ya Ndege ya Bakhmut.

"Vita vya miinuko mikubwa kwenye ubavu kaskazini na kusini mwa vitongoji vinaendelea," alisema.

Naye Mkuu wa shirika la nishati ya atomiki la Umoja wa Mataifa (IAEA), Rafael Grossi, alisema kuwa mtambo wa nyuklia wa Zaporizhzhya umekatwa kabisa kutoka kwenye ugavi wa nje wa umeme, hali ambayo inauweka usalama wa nyuklia kiwandani hapo katika hatari kubwa.

Kampuni ya nyuklia ya Ukraine Enerhoatom ilithibitisha tukio hilo kwenye kiwanda hicho kinachokaliwa na wanajeshi wa Russia kusini mwa Ukraine, ikisema kwamba kiwanda hicho kiliharibiwa kwa shambulio.

Vile vile, Ukraine ilisema kuwa tayari imekiunganisha tena kiwanda hicho kwenye ugavi wa nje wa umeme. **DW**

## Kenya na Uganda kutafuta mfadhili mradi wa reli

**KAMPALA,** Uganda

MAOFISA wa Kenya na Uganda wamesema kwamba kwa sasa nchi hizo zitalazimika kutafuta mfadhili mbadala kwa ajili ya mradi wa reli ya kisasa itakayounganisha mji wa Naivasha na Kampala kupitia Malaba.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa kwenye gazeti moja la ukanda The East African, ofisa mmoja katika wizara ya ujenzi nchini Uganda, alithibitisha juu ya kuanza mchakato wa nchi zao kutafuta mfadhili kutoka nchi za Ulaya, licha ya kutobainisha taifa lengwa.

Alieleza kuwa hatua hiyo inamaanisha kuwa maendeleo ya mradi wa reli ya kilometa 273 ambayo ujenzi wake ulisimama kwa muda, sasa utafufuliwa na itatokea jijini Kampala Uganda hadi kwenye mji wa Mombasa nchini kenya.

Hata hivyo, wakati Uganda ikijaribu kutafuta wafadhili zaidi, Kenya kwa upande wake imesema tayari ina deni kubwa la kulipa kwa nchi ya China na kwamba haina mpango wa kukopa zaidi kutoka kwa taifa hilo licha ya kudaiwa kuwa wamekuwa kwenye mazungumzo ya kuangalia uwezekano wa kupata mkopo wenye masharti nafuu.

Aidha, hayo yanajiri baada ya juma lililopita, Uganda kudai kuwa ujenzi wa reli hiyo utakaogharibu dola za Marekani Bilioni 2.2 utaanza tena mwaka huu, baada ya mazungumzo yake na serikali ya China kuhusu kupewa mkopo kugonga mwamba. **RFI**



Mahema yaliyotengenezwa kwa kanga na raia wa Sudan huko Chad na Sudan Kusini baada ya kikimbia taifa lao wakihofiwa mapigano yanayoendelea. **PICHA: AP**

## Mkataba usitishaji mapigano watarajiwa Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

MKATABA wa kusitisha mapigano nchini Sudan unatarajiwa kuanza rasmi utekelezaji wake baada ya tarehe ya makubaliano ya kusitisha kufikiwa jana, licha ya kuendelea kuripotiwa mapigano katika baadhi ya maeneo, hali inayoibua maswali kwamba mkataba huo utadumu.

Makubaliano ya kusitisha mapigano, yalitiwa saini na wawakilishi wa jeshi na wale wa wapiganaji wa kikosi cha Msaada wa Haraka (RSF), baada ya mazungumzo yaliyofanyika nchini Saudi Arabia na sasa yataanza kutekelezwa rasmi kuanzia jana Jumatatu.

Ilielezwa kuwa katika makubaliano hayo, mbali na usitishwaji wa mapigano, pande hizo mbili zitatakiwa kuruhusu kufikishwa kwa misaada ya kibinadamu kwa raia walionaswa kwenye mapigano.

Hata hivyo, wachambuzi wa masuala mbalimbali walisema, haifahamiki ikiwa mkuu wa majeshi ya Sudan Jenerali Abdel al Burhani na mwenzake anayeoongoza kundi la RSF Mohamed Dagalo, watakuwa tayari kuheshimu makubaliano ya safari hiyo.

Aidha, hayo yalijiri wakati Umoja wa Mataifa (UN) ukisema hadi kufikia mwishoni mwa juma lililopita, watu zaidi ya milioni 1.1 wamekimbia makazi yao na wengine kuwa wakimbizi kwenye nchi jirani.

Ilibainishwa kuwa pande hizo hasimu za kijeshi zimekuwa zikisisitiza kuendelea na vita, kila mmoja akidai kuwa lengo lake ni kuibuka mshindi katika vita ya kuwania madaraka yanyoendelea na ambayo imeingia wiki ya sita. **RFI**

# MTIBWA KUZIGEUZA 'NGAZI' KAGERA SUGAR, GEITA KUKWEPA 'PLAY OFF'

Na Hadija Mngwai

KLABU ya Mtibwa Sugar imetangaza vita katika mechi mbili zilizobakia za Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar na Geita Gold kuhakikisha inashinda mechi hizi na kukwepa kucheza mechi za 'play off' kuwanuia kubaki Ligi Kuu msimu ujao.

Mtibwa Sugar ipo nafasi ya 14 ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 29 sawa na KMC ambazo zote zipo katika hatari ya kucheza mechi za mtoano iwapo zitamaliza katika nafasi hizo.

**Mtibwa Sugar itashuka dimbani kesho kucheza dhidi ya Kagera Sugar katika Uwanja wa Manungu kisha itamalizia ligi kwa kucheza na Geita Gold Juni 9, awali mchezo huo wa mwisho ulikuwa uchezwe Mei 28 lakini Bodi ya Ligi imefanya marekebisho ya ratiba na mechi za mwisho za Ligi Kuu msimu huu zitachezwa Juni 9.**

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, amesema kuwa, Mtibwa ipo katika huzuni kubwa kwa sasa kutokana na kucheza mechi za 'play off' misimu miwili mfululizo hivyo wanajipanga kuhakikisha wanashinda michezo miwili iliyobakia ili kuondoka katika nafasi hiyo.

"Mtibwa Sugar tumefanya vibaya misimu mitatu mfululizo, misimu miwili ya 2021/22 na 2022/23 tumecheza mechi za play off hata msimu huu pia hatukucheza vizuri. Tunajipanga kutumia mechi zetu mbili zilizobakia dhidi ya Kagera Sugar Jumatano (kesho) tuvune alama tatu na kisha tumalizie vizuri na Geita Gold ili kuweza kuepuka kucheza mechi za mtoano," alisema Kifaru.

Aidha, alisema Mtibwa Sugar ni miongoni mwa timu kongwe ambayo haijashuka daraja tangu ipande mwaka 1995 ikiwa ni miongoni mwa timu iliyozalisha nyota wengi akiwamo Dickson Job na Kibwana Shomari hivyo ikishuka italeta huzuni kwa nyota wengi.




Wachezaji wa timu ya vijana wanaolelewa na Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam wakifanya mazoezi jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yaipongeza TFF kusimamia soka

Na Shufaa Lyimo

SERIKALI kupitia kwa Naibu Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma, imelipongeza Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kwa jinsi inavyosimamia vema maendeleo ya mpira wa miguu hapa nchini.

Akizungumza na gazeti la Nipashe hivi karibuni alisema TFF imefanya kazi kubwa kwani kwa sasa Tanzania inafahamika kupitia mpira.

"Ninaipongeza TFF kwa kweli imefanya kazi kubwa kuhakikisha mpira wetu unafika mbali tunaona jinsi ambavyo Ligi yetu inavyofanya vizuri viongozi wanastahili pongezi, kwa sasa kwenye ramani ya soka Tanzania imeanza kufahamika na pengine kuogopwa kwa namna klabu zetu zinavyofanya vizuri," alisema Mwinjuma.

Hata hivyo Naibu Waziri huyo amelitaka Shirikisho hilo kuongeza juhudi zaidi ya kupinga rushwa michezoni.

"TFF iongeze juhudi ya kupinga vitendo vya rushwa michezoni na kwa atakayebainika anachukua rushwa wamchukulie hatua kali za kinidhamu kwa mujibu wa kanuni na sheria za nchi ili iwe fundisho,"alisema Mwinjuma.

Katika hatua nyingine, Mwijuma ameitaka Klabu ya Yanga kuhakikisha inafanya vema katika mchezo wake wa kwanza wa fainali wa kombe la Shirikisho barani Afrika dhidi ya USMA Alger Mei 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam.

Aidha alisema Yanga imefanya kazi kubwa mpaka kufikia hatua hiyo ya fainali na kuwataka Watanzania wajitokeze kwa wingi uwanjani siku ya mchezo ili kuwapa morali wachezaji waweze kufanya vizuri na kuendelea kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania.

## Mashujaa yasogelea kucheza Ligi Kuu

Na Adam Fungamwango

USHINDI wa mabao 4-0 walioupata juzi Mashujaa FC dhidi ya timu kongwe ya Pamba FC ya Mwanza umeifanya timu hiyo ya Kigoma kusogelea kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Mashujaa sasa watalazimika kutafuta sare au ushindi wowote kwenye mchezo wa marudiano kuweza kucheza mchezo mwingine wa 'Play Off' dhidi ya mshindi wa mchezo kama huo kwa timu za Ligi Kuu zitakazoshika nafasi ya 13 na 14 kutafuta nafasi moja ya kubaki au kupanda Ligi Kuu.

Matokeo hayo ya juzi kwenye Uwanja wa Tanganyika mjini Kigoma hayakutarajiwa na wengi kutokana na ubora wa Pamba FC ambayo ilimaliza Ligi daraja la kwanza ikiwa kwenye nafasi ya tatu na pointi zake 59 ikizidiwa kwa pointi moja tu na Kitayose ya Tabora ambayo imepanda daraja moja kwa moja ikiungana na JKT Tanzania.

Katika mchezo huo wa juzi, Pamba ilikuwa ikipewa nafasi kubwa ya kuibuka na ushindi lakini wakakumbana na matokeo ya kushtukiza kwa kuambulia kipigo hicho.

Mechi ya marudiano kati ya timu hizo mbili itachezwa Jumapili ijayo kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

Timu zitakazomaliza nafasi ya 13 na 14 kwenye Ligi Kuu nazo zitacheza mechi ya mchujo 'play off' kupata timu itakayocheza na Mashujaa FC.

## Yanga tishio hadi Ligi ya U-17

Na Adam Fungamwango

WAKATI timu ya wakubwa ikiwa imetwaa ubingwa, imetinga fainali ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika na Kombe la FA, timu ya Yanga chini ya miaka 17 inaongoza kwenye msimamo wa Ligi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), kwa vijana chini ya umri huo inayoendelea kutimua vumbi kwenye Uwanja wa Kituo cha Ufundi TFF, Kigamboni.

Vijana wa Yanga wanaonekana kutaka kufanya kama kaka zao, kwani mbali na kuongoza, lakini wamekuwa wakitoa vipigo vikubwa kwenye ligi hiyo na kuwafanya kuongoza kwenye msimamo.

Baada ya kuitwanga JKT Tanzania juzi mabao 4-1, inaongoza ligi ikiwa na pointi 12, ikishinda mechi zote nne ilizocheza, ikifunga mabao 19 na kuruhusu bao moja pekee.

Azam FC, baada ya kuifunga Ruvu Shooting mabao 4-1, iko kwenye nafasi ya pili ya msimamo nayo ikiwa imecheza mechi nne na kushinda zote, lakini ikiwa na mabao 13 na kufungwa moja.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### VLAHOVIC ATAKIWA JUVE

CHELSEA imewasilisha ofa ya Euro milioni 80 kwa Juventus kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic, 23. ***(ESPN)***

### ...MAN UNITED NAO WAMTAKA

MANCHESTER United pia wanaandaa ofa rasmi kwa ajili ya Dusan Vlahovic, ambaye ameweka wazi kuwa anataka kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. ***(Football Transfers)***

### POTTER ATAKIWA LEICESTER

KLABU ya Leicester City inapanga kuwasiliana na kocha wa zamani wa Brighton na Chelsea, Graham Potter kuhusu kuwa kocha wao wa kudumu. ***(Football Insider)***

### MOURINHO AMTAKA YOURI

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho anataka kumsajili kiungo wa kati wa Ubelgiji, Youri Tielemans, 26, mara mkataba wa mchezaji huyo utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. ***(Gazzetta dello Sport)***

### NEVES CHAMBO KWA FATI

BARCELONA imefikia makubaliano na wakala Jorge Mendes kuhusu uhamisho wa kiungo wa Wolves, Ruben Neves, 26, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno akitarajiwa kuhamia Nou Camp kama sehemu ya makubaliano ya kubadilishana na mshambuliaji wa Hispania, Ansu Fati, 20. ***(Sport)***

### MARTIAL AWANIWA VILLA

KLABU ya Aston Villa inatafakari uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa Manchester United na Ufaransa, Anthony Martial, 27, kwa mkopo msimu ujao. ***(Football Transfers)***

### LERMA AWINDWA

KLABU ya Crystal Palace ina nia ya kumnunua kiungo wa kati wa Bournemouth na Colombia, Jefferson Lerma, 28, huku mkataba wa mchezaji huyo ukitarajiwa kumalizika msimu huu. ***(Sun)***

### HENDERSON MKATABA MPYA

KLABU ya Nottingham Forest inataka kumpatia mkataba wa kudumu kipa wa Manchester United na England aliyejiunga nao kwa mkopo, Dean Henderson, 26. ***(Telegraph)***

### CITY YAMTAKA STEFFEN

KLABU ya Manchester City iko tayari kumuuza mlinda mlango, Zack Steffen, 28, msimu huu wa joto wakati muda mkopo wa Mmarekani huyo akiwa Middlesbrough utakapomalizika. ***(Sun)***

### DIARRA AWANIWA

ASTON Villa na Wolves zinamwania kiungo wa kati Mfaransa, Habib Diarra, 19 kutoka Strasbourg, ambaye thamani yake ni pauni milioni 20. ***(Sun)***

### ATAKIWA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United wanajadiliana kuhusu uwezekano wa kurefusha mkataba wa winga wa Uruguay, Facundo Pellistri, 21, hadi Juni 2028. ***(Fabrizio Romano)***

## DON ZA SOKA MAGA YA ULAYA



# MAN CITY HAIJAKAMILIKA BILA LIGI YA MABINGWA–GUARDIOLA

**MANCHESTER,** England

●●● Alitwaa taji lake la tano la EPL ndani ya miaka sita baada ya ushindi wa 1-0 dhidi ya...

PEP Guardiola amesema timu yake ya Manchester City italazimika kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya ili ichukuliwe kuwa moja ya klabu bora zaidi ya wakati wote.

**Guardiola alitwaa taji lake la tano la Ligi Kuu ya England ndani ya miaka sita baada ya ushindi wa 1-0 dhidi ya Chelsea Jumapili kwenye Uwanja wa Etihad, kazi aliyoiita "ya kipekee."**

Umeanza mjadala kuhusu iwapo City tayari imepata nafasi kati ya timu bora zaidi katika historia, lakini Guardiola alisema itabidi washinde kwanza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Sikuweza kufikiria kushinda taji la Ligi la tano ndani ya miaka sita," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari baada ya kunyanyua kombe hilo Jumapili.

"Nina hisia tumefanya jambo la kipekee, lakini ili kuzingatiwa kuwa moja ya timu kubwa lazima tushinde Ligi ya Mabingwa Ulaya, vinginevyo hatujakamilika."

City wana nafasi ya kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza watakapocheza na Inter Milan katika fainali Juni 10, mwaka huu.

Pia wanajiandaa kwa fainali ya Kombe la FA dhidi ya Manchester United huku wakipanga kutwaa mataji matatu ya msimu huu.

"Wachezaji wanapaswa kusherehekea, lakini ni wakati wa kupumzika kiakili kwa fainali na tunapaswa kucheza michezo miwili zaidi katika Ligi Kuu na kujaribu kuwa tayari," aliongeza Guardiola.

"Sasa nina hisia kwamba tumechoka kidogo na imekuwa safari ndefu. Kuna tabia ya kufikiria kuwa imekamilika, lakini kwa matumaini inaweza kupita haraka."

Wakati wa kusherehekea ubingwa, Guardiola pia alimpongeza kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, ambaye alikuwa msaidizi wake wa zamani hapo City. Arsenal waliongoza kwenye msimamo kwa pointi nane mapema Aprili, lakini hawakuweza kuendana na timu ya Guardiola katika mbio hizo.

"Kwa uhusiano nilionao na Mikel, hongera kwa walichokifanya," alisema Guardiola. "Amewarudisha kama Arsenal ya zamani.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,117,4

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 24 NA 25 MEI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 24/05/23 | 20:00 | Djurgardens IF vs BK Hacken | 2.30 | 3.39 | 2.62 |
| 02. 24/05/23 | 21:45 | Ross County vs St Johnstone | 2.37 | 3.15 | 2.89 |
| 03. 24/05/23 | 21:45 | Livingston vs Motherwell | 2.89 | 3.10 | 2.40 |
| 04. 24/05/23 | 21:45 | Dundee Utd vs Kilmarnock | 2.38 | 3.20 | 2.83 |
| 05. 24/05/23 | 23:00 | Espanyol vs Atletico Madrid | 2.75 | 3.35 | 2.33 |
| 06. 25/05/23 | 01:00 | Patronato Parana vs Olimpia Asuncion | 2.47 | 3.12 | 2.67 |
| 07. 25/05/23 | 01:00 | Juventude RS vs Atletico GO | 2.36 | 3.17 | 2.77 |
| 08. 25/05/23 | 01:00 | Londrina PR vs Ceara CE | 2.70 | 3.05 | 2.50 |
| 09. 25/05/23 | 03:30 | Criciuma SC vs Sport Recife | 2.34 | 3.02 | 2.92 |
| 10. 25/05/23 | 05:00 | FBC Melgar vs Atletico Nacional | 2.32 | 3.17 | 2.83 |
| 11. 25/05/23 | 20:30 | Mallorca vs Valencia | 3.40 | 2.95 | 2.19 |
| 12. 25/05/23 | 20:30 | Ankaragucu vs Basaksehir | 2.64 | 3.31 | 2.39 |
| 13. 25/05/23 | 21:30 | Grasshoppers vs St. Gallen | 2.49 | 3.57 | 2.49 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# DORTMUND YANUSA UBINGWA BUNDESLIGA

**DORTMUND,** Ujerumani

BORUSSIA Dortmund wamebakiwa na ushindi mmoja kunyakua taji la Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, baada ya ushindi wa 3-0 dhidi ya Augsburg, Jumapili.

Kupoteza kwa Bayern Munich kwa Leipzig siku ya Jumamosi kulifungua mlango kwa Dortmund na wakachukua nafasi yao, na kuwa na nafasi ya kumaliza utawala wa miaka 10 wa klabu hiyo ya Bavaria kama mabingwa wa Ujerumani.

Sebastian Haller - ambaye alikosa kipindi cha kwanza cha msimu alipokuwa akipambana na saratani - alifunga mara mbili na Julian Brandt moja baada ya Felix Uduokhai kutolewa nje kwa kadi nyekundu kwa upande wa Augsburg.

Ushindi dhidi ya Mainz katika siku ya mwisho ya msimu Jumamosi ijayo utaifanya Dortmund kunyakua taji lao la kwanza la Bundesliga kwa kipindi cha miaka 11.

Wao Mainz walipokea kichapo cha mabao 4-1 nyumbani kwa Stuttgart siku ya Jumamosi licha ya kuchukua uongozi, huku Lars Stindl akifunga bao la kusawazisha dakika ya 90 na kuifanya Borussia Monchengladbach kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi Bayer Leverkusen.

# Vinicius Jr adai La Liga ni ligi ya wabaguzi

**MADRID,** Hispania



MCHEZAJI wa Real Madrid, Vinicius Junior amesema Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, "ni ya wabaguzi wa rangi" baada ya kushambuliwa kwa maneno ya kibaguzi huko Valencia, Jumapili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alitolewa kwa kadi nyekundu baada ya kufanya vurugu katika dakika 97 akizozana na Hugo Duro, wakati Madrid walipokubali kichapo cha bao 1-0.

Mapema katika mchezo huo, Vinicius aliyepandwa na hasira alijaribu kumfahamisha mwamuzi kuhusu vitendo vya mashabiki wa Valencia.

"Michuano ambayo hapo awali ilikuwa ya Ronaldinho, Ronaldo, Cristiano na Messi leo ni ya wabaguzi wa rangi," aliandika Vinicius kwenye Instagram yake.

"Haikuwa mara ya kwanza, wala ya pili, wala ya tatu. Ubaguzi wa rangi ni jambo la kawaida kwenye La Liga. Wasimamizi wa mashindano hayo wanafikiri ni jambo la kawaida, Shirikisho na wapinzani pia wanaendekeza suala hili.

"Taifa zuri, ambalo lilinikaribisha na ninalipend[...] lakini limekubali kuonekan[...] kama nchi ya kibaguzi d[...]niani. Samahani kwa Wahi[...]pania ambao hawakubalia[...] na mimi, lakini leo hii hu[...] Brazil, Hispania inajulikan[...] kama nchi ya wabaguzi.

"Cha kusikitisha kwa baha[...] mbaya ni kitu kinachotok[...] kila wiki, sina mtete[...] Ninakubali. Lakini nina ng[...]vu na nitaenda hadi mwish[...] kupaza sauti dhidi ya wab[...]guzi. Hata kama ni mbali [...] hapa."

Katika taarifa yake, LaLi[...] ilisema imekuwa "ikipigan[...] na aina hii ya tabia kwa mi[...]ka mingi, pamoja na kuku[...] maadili chanya ya michez[...] sio tu kwenye uwanja, laki[...] pia nje ya mchezo."

17,539/-

# NABI AWAGEUKIA USM ALGER

**Na Shufaa Lymio**

BAADA ya kufanikiwa kutinga hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka Tanzania, TFF (ASFC), Kocha wa Yanga Nasreddine Nabi amesema sasa wanaelekeza nguvu zao zote kwenye mchezo wa kwanza wa fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya USM Alger utakaochezwa Mei 28 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Nabi alisema baada ya kuifunga Singida Big Stars juzi na kutinga fainali ya FA, sasa akili zao na nguvu wanazielekeza kwenye mchezo huo wa fainali dhidi ya wababe hao kutoka Algeria.

**"Huu mchezo dhidi ya Singida Big Stars ulikuwa mchezo muhimu sana kwetu, tulikuwa na muda mfupi wa kujiandaa tangu kutoka Afrika Kusini, jambo lililojema tumepata ushindi, ushindi huu unatupa hali ya kupambana kwenye mchezo wetu wa kimataifa, tunaelekeza akili zetu na nguvu kwenye mchezo huu wa Mei 28," alisema Nabi.**

Alisema wachezaji wake wote wana morali ya juu hasa baada ya ushindi dhidi ya Singida Big Stars na sasa mawazo yao yapo kwenye mchezo dhidi ya USM Alger.

Kocha huyo alisema amewafuatilia wapinzani wake kufuatia michezo mbali mbali waliyoicheza na kubaini kuwa ni timu ambayo wanapaswa kucheza nayo wakiwa na tahadhari kubwa.

"USM Alger ni timu kubwa na wana uzoefu wa mashindano ya kimataifa, nimewafuatilia na tunatakiwa kuwa na utulivu na tahadhari kubwa kwenye mchezo wetu tutakapokutana nao, mchezo wa nyumbani ni mchezo muhimu zaidi," alisema Nabi.

Aidha, alisema Watanzania wajitokeze kwa wingi siku ya mchezo huo ili kuzidi kuwapa hamasa mashujaa wao ambao wanataka kuweka historia kwa Tanzania kutwaa ubingwa wa Kombe la Afrika msimu huu.

"Katika mchezo uliopita na Singida Big Stars nilipumzisha baadhi ya wachezaji kwa kuwa nafahamu tunajiandaa na mchezo wetu wa fainali Kombe la Shirikisho Afrika hivi karibuni hivyo mashabiki waondoe hofu, tumejipanga na tunaendelea kujiandaa," alisema Nabi.

Baada ya mchezo wa kwanza wa fainali utakaochezwa Mei 28 hapa nchini, Yanga itasafiri kwenda Alger, Algeria kucheza mchezo wa marudiano Juni 3 utakaoamua bingwa wa michuano hiyo msimu huu.

## Robertinho aomba kushirikishwa hatua zote

INATOKA UK. 23

ambacho tumeweza kukipata.

" Kuhusu suala la usajili tayari tumeanza mikakati kwa sababu tunaelewa tumekosea wapi na kitu gani tunapaswa kufanya ili tuweze kuwa bora msimu ujao hivyo ni jambo jema kuweza kutambua kila hatua ya usajili wa wachezaji ambao tumelenga kuwasajili kupitia viongozi na ripoti itakavyoweza kuonyesha mahitaji yetu ya msimu ujao, " alisema Robertinho.

Alisema kwa sasa wanaangalia michezo miwili iliyobakia na amewataka wachezaji wake kupambana kushinda mechi mbili zilizosalia ili kumaliza ligi hiyo kwa heshima.

Kikosi cha Simba kinaendelea na mazoezi katika uwanja wa Mo Simba Arena kujiandaa na michezo hiyo miwili dhidi ya Polisi Tanzania utakaopigwa Juni 6 na ule dhidi ya Coastal Union utakaochezwa Juni 9, michezo yote itachezwa jijini Dar es Salaam.




Mchezaji wa timu ya wenye ulemavu, Samson Ponza, akirusha Tufe wakati akifanya mazoezi jana katika Viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Rais Samia anunua tiketi 5,000 Yanga*

INATOKA UKURASA 24

hiyo ili iende Algeria katika mechi yao ya marudiano.

Yanga imekuwa kwenye kiwango bora msimu huu ikifanikiwa kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu na kuingia kwenye fainali mbili za kombe la Shirikisho la TFF na lile la CAF.


# SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 27/05/23 | 19:00 | ACF Fiorentina vs AS Roma | 2.42 | 3.15 | 2.80 |
| 02. 27/05/23 | 20:00 | Sevilla FC vs Real Madrid | 2.80 | 3.45 | 2.25 |
| 03. 27/05/23 | 22:00 | Montpellier HSC vs OGC Nice | 2.47 | 3.30 | 2.60 |
| 04. 28/05/23 | 02:30 | Orlando City SC vs Atlanta United FC | 2.15 | 3.10 | 2.85 |
| 05. 28/05/23 | 15:30 | Fortuna Sittard vs NEC Nijmegen | 2.50 | 3.40 | 2.50 |
| 06. 28/05/23 | 15:30 | AZ Alkmaar vs PSV Eindhoven | 2.55 | 3.50 | 2.40 |
| 07. 28/05/23 | 15:30 | Carlisle United vs Stockport County FC | 3.00 | 3.15 | 2.28 |
| 08. 28/05/23 | 16:00 | AC Monza vs US Lecce | 2.55 | 3.05 | 2.70 |
| 09. 28/05/23 | 17:15 | Racing Santander vs FC Cartagena | 2.60 | 3.05 | 2.65 |
| 10. 28/05/23 | 17:30 | Rio Ave FC vs FC Famalicao | 2.50 | 3.15 | 2.65 |
| 11. 28/05/23 | 18:30 | Aston Villa vs Brighton & Hove Albion | 2.19 | 3.50 | 2.85 |
| 12. 28/05/23 | 18:30 | Chelsea FC vs Newcastle United | 2.80 | 3.35 | 2.30 |
| 13. 28/05/23 | 18:30 | Leeds United vs Tottenham Hotspur | 2.65 | 3.45 | 2.35 |
| 14. 28/05/23 | 20:00 | Getafe CF vs CA Osasuna | 2.40 | 3.25 | 2.75 |
| 15. 28/05/23 | 20:00 | Cadiz CF vs RC Celta de Vigo | 2.60 | 3.25 | 2.50 |
| 16. 28/05/23 | 20:00 | Girona FC vs Real Betis Seville | 2.60 | 3.10 | 2.65 |
| 17. 28/05/23 | 21:45 | Juventus Turin vs AC Milan | 2.24 | 3.20 | 3.00 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 23/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:35 | 3089 | Nantong Zhiyun vs Wuhan Three Towns FC | 5.14 | 3.70 | 1.55 |
| 14:35 | 4296 | Chengdu Qianbao vs Shanghai Shenhua | 1.92 | 3.29 | 3.50 |
| 14:35 | 4861 | Changchun Yatai vs Qingdao Hainiu | 1.86 | 3.39 | 3.60 |
| 14:35 | 5183 | Beijing Guoan vs Shijiazhuang | 1.49 | 3.76 | 5.76 |
| 15:00 | 4971 | Hawassa Kenema SC vs Ethiopian Medhin | 2.70 | 3.06 | 2.49 |
| 15:15 | 1713 | Sabah vs Perak FA | 1.18 | 5.97 | 10.29 |
| 15:30 | 1556 | WIT Georgia vs FC Spaeri | 3.33 | 3.54 | 1.93 |
| 16:00 | 5201 | Kelantan FA vs Pdrm | 2.14 | 3.45 | 2.83 |
| 16:00 | 5621 | Negeri Sembilan vs Kelantan United FC | 1.31 | 4.84 | 7.21 |
| 17:30 | 1123 | Chador Malu Yazd vs Khalijfars Mahshahr | 1.65 | 3.05 | 4.80 |
| 17:30 | 1152 | Saipa Karadj vs Esteghlal Mollasani | 1.70 | 2.95 | 4.60 |
| 17:30 | 2389 | Pars Jonoubi Jam vs Shahrdari Astara | 1.90 | 2.86 | 4.47 |
| 17:30 | 2822 | Esteghlal Khuzestan vs Arman Gohar Sirjan | 1.40 | 3.70 | 6.40 |
| 17:30 | 3554 | Mes Shahr-e Babak vs Fajr Sepasi | 2.90 | 2.49 | 2.55 |
| 17:30 | 5875 | Chooka Talesh FC vs Caspian Babol | 2.75 | 2.65 | 2.55 |
| 18:00 | 2862 | FS Metta/Lu vs SK Super Nova | 1.46 | 4.22 | 5.56 |
| 18:00 | 3902 | Ethiopia Electricity vs Mekelakeya | 4.30 | 3.15 | 1.68 |
| 18:30 | 2345 | Al Suwaiq vs Sohar Club | 1.77 | 2.95 | 4.20 |
| 18:30 | 2463 | Oman Club vs Al Oruba | 1.90 | 2.95 | 3.65 |
| 18:30 | 2660 | Sur vs Al Nahda (Oman) | 6.20 | 3.41 | 1.55 |
| 18:30 | 2910 | Rustaq Club vs Al Seeb | 3.35 | 2.80 | 2.06 |
| 18:30 | 3397 | Dhofar Salalah vs AL Etihad | 1.37 | 4.10 | 7.89 |
| 18:30 | 4417 | Sport Podbrezova vs Ruzomberok | 2.61 | 3.22 | 2.40 |
| 18:30 | 4992 | Al Nasr Salalah vs Bahla | 2.11 | 2.75 | 3.30 |
| 18:30 | 5018 | Dukla Banska Bystrica vs MSK Zilina | 2.08 | 3.55 | 2.88 |
| 18:30 | 5953 | AL Musanaa vs AL Bashair | 1.59 | 3.20 | 5.00 |
| 19:00 | 3441 | Aswan vs National Bank | 2.72 | 2.97 | 2.62 |
| 19:00 | 3616 | Doxa Katokopia vs Nea Salamis | 1.75 | 3.69 | 4.22 |
| 19:00 | 3710 | AL Adalh vs Al Hilal Riyadh | 6.62 | 4.91 | 1.40 |
| 19:00 | 4058 | Karmiotissa vs Anorthosis Famagusta | 2.69 | 3.27 | 2.48 |
| 19:00 | 5325 | Kiffen vs Klubi 04 | 4.56 | 3.94 | 1.60 |
| 19:45 | 2983 | VVV Venlo vs Willem II Tilburg | 3.30 | 3.35 | 2.04 |
| 20:00 | 1368 | Slovacko vs Sparta Prague | 3.33 | 3.43 | 2.05 |
| 20:00 | 1840 | Sigma Olomouc vs Slavia Prague | 5.30 | 4.08 | 1.55 |
| 20:00 | 4686 | Viktoria Plzen vs Bohemians | 1.52 | 4.21 | 5.47 |
| 20:00 | 5566 | Orgryte IS vs GIF Sundsvall | 1.85 | 3.62 | 3.94 |
| 20:30 | 2539 | Celta Vigo vs Girona | 1.97 | 3.40 | 3.46 |
| 20:30 | 3264 | Real Sociedad vs Almeria | 1.43 | 4.41 | 6.02 |
| 20:30 | 3621 | Taby FK vs FC Stockholm Internazionale | 2.30 | 3.54 | 2.55 |
| 21:15 | 1102 | Lausanne-Sport vs FC Wil | 1.88 | 3.54 | 3.39 |
| 21:15 | 1620 | FC Vaduz vs FC Stade LS Ouchy | 2.82 | 3.54 | 2.11 |
| 21:15 | 1746 | Yverdon-Sport FC vs FC Aarau | 2.30 | 3.50 | 2.57 |
| 21:15 | 4128 | AC Bellinzona vs FC Thun | 4.82 | 3.95 | 1.54 |
| 21:15 | 5411 | FC Schaffhausen vs Neuchatel Xamax | 2.14 | 3.54 | 2.77 |
| 21:30 | 1939 | Farco FC vs Smouha Club | 2.53 | 2.83 | 2.98 |
| 21:30 | 2701 | Al Ittihad Jeddah vs AL Baten | 1.19 | 6.64 | 12.85 |
| 21:30 | 3628 | Al Ahly Cairo vs Enppi Club | 1.33 | 4.72 | 8.43 |
| 21:30 | 5981 | Al Nasr Riyadh vs Al Shabab Riyadh | 1.64 | 4.05 | 4.69 |
| 22:00 | 1302 | NAC Breda vs Maastricht | 1.63 | 3.85 | 4.60 |
| 23:00 | 3769 | Valladolid vs Barcelona | 3.29 | 3.48 | 2.00 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Mei 23, 2023

Nipashe




Dortmund yanusa ubingwa Bundesliga UKURASA 22




Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa (kulia), akikabidhi Sh. milioni 20 kwa makamu wa Rais wa klabu ya Yanga, Arafat Haji, ikiwa ni zawadi ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa magoli mawili waliyofunga katika ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya wenyeji, Marumo Gallants kwenye mchezo wa marudiano wa nusu fainali Kombe la Shirikisho Afrika wiki iliyopita nchini Afrika Kusini. **PICHA: BINZUBERY**

# Rais Samia anunua tiketi 5,000 Yanga

## ●●● Ni kwa ajili ya mashabiki kwenda kuwashangilia 'Wananchi' Mei 28...

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amejitoa kimasomaso kuhakikisha kuwa Yanga inashinda nyumbani dhidi ya USM Alger ya Algeria kwa kununua tiketi 5,000 ili mashabiki waingie kwa wingi uwanjani.

**Mechi hiyo ya fainali inayosubiriwa kwa hamu imepangwa kupigwa Mei 28 katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, ikiwa ni mechi ya mkondo wa kwanza wa Kombe la Shirikisho.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema tiketi hizo ni mwendelezo wa kuongeza hamasa, ikiwa ni baada pia ya kuahidi Sh. milioni 20 katika kila bao la ushindi litakalofungwa na wachezaji wa Yanga kwenye mechi hizo mbili za fainali.

"Rais Samia anahakikisha kuwa Yanga inachukua kombe kwa kuendeleza hamasa hizi za kununua tiketi 5,000 kwa lengo la kuujaza Uwanja wa Taifa utakaoshuhudia mchezo mgumu wa fainali kati ya timu ya Tanzania ya Yanga dhidi ya USM Alger.

"Rais anawataka Watanzania waende kuujaza uwanja kwa sababu mama hana mbambamba katika mbio za Yanga kuitangaza nchi kimataifa kupitia mpira wa miguu," alisema.

Katika hatua nyingine, Msigwa aliwataka wachezaji kuingia uwanjani kwa nguvu zote ili washinde magoli mengi kwa sababu fedha za Rais zinazotolewa ili kuibua hamasa bado zipo kwa lengo moja la kuhakikisha Yanga inaibuka kidedea katika mechi zake za fainali za Kombe la Shirikisho.

Mechi ya marudiano kati ya Yanga na USM Alger inatarajiwa kupigwa nchini Algeria, Juni 3, mwaka huu, huku Yanga ikiingia fainali kwa mara ya kwanza katika historia ya michuano ya Kimataifa inayoendeshwa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika.

Mengine makubwa yaliyofanywa na Rais Samia dhidi ya Yanga katika mechi yao ya fainali ni kuipa ndege klabu

INAENDELEA UKURASA 23

# Robertinho aomba kushirikishwa hatua zote usajili Simba

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Simba, Robert Oliveira 'Robertinho', amewaambia mabosi wa timu hiyo anataka ashirikishwe katika kila hatua ya usajili watakaofanya kuelekea msimu ujao baada ya kukabidhi faili la majina ya wachezaji anaowataka kwenye kikosi chake.

Robertinho ametoa kauli hiyo kufuatia Simba kukosa makombe yote msimu huu licha ya kuonyesha upinzani mkali mbele ya wapinzani wao Yanga.

Yanga wamefanikiwa kushinda ubingwa wa Ligi Kuu Bara kwa mara ya pili mfululizo huku wakifanikiwa kuingia fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika na Kombe la FA.

Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho alisema anataka ashirikishwe kwenye hatua ya usajili ili kupata wachezaji anaowataka kwenye kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao watakaomwezesha kufikia malengo.

Msimu huu Simba walikuwa na malengo ya angalau kucheza hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kombe la Shirikisho (FA), hata hivyo wameshindwa kufikia malengo hayo na kushuhudia watani zao, Yanga wakichukua ubingwa wa Ligi Kuu na kutinga hatua ya fainali katika michuano ya Shirikisho Afrika na ile ya FA.

"Nashukuru Mungu kwa sasa tunasubiria kumaliza msimu kwa mechi mbili zilizobakia kabla ya kuanza maandalizi ya msimu ujao, ingawa tumeanza mikakati mapema ya kujua mahitaji gani ambayo tunaweza kuyahitaji kuelekea msimu ujao kwa sababu msimu huu hakuna

INAENDELEA UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >